NDAKI YA ELIMU
SKULI YA ELIMU

# ATHARI ZA KIFONOLOJIA ZA KINYARWANDA KATIKA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI: MFANO WA SHULE ZA SEKONDARI TEULE WILAYANI BUGESERA, RWANDA

**na**

**Bigirimana Jean de Dieu**

**Nambari ya Usajili: 222013917**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA MAHITAJI YA SHAHADA YA UMAHIRI WA ELIMU KATIKA KISWAHILI NA ELIMU YA CHUO KIKUU CHA RWANDA, NDAKI YA ELIMU**

**OKTOBA, 2024**

# IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, **Bigirimana Jean de Dieu**, ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu ya asilia na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada yoyote.

Tarehe: …/10/2024

(Mwanafunzi)

# ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Waliotia saini hapa chini wanathibitisha kwamba tasnifu yenye anwani "**Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Ujifunzaji wa Kiswahili: Mfano wa Shule wa Sekondari Teule katika Wilaya ya Bugesera, Rwanda**" iliandikwa chini ya usimamizi wao na wanapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri wa Elimu katika Kiswahili na Elimu.

Dkt. Wallace Kapele Mlaga (PhD)

(Msimamizi Na: 1)

Tarehe: …/10/2024

---------------------------------------------------------------------------

Bw. Niyirora Emmanuel

(Msimamizi Na: 2)

Tarehe: …/10/2024

## SHUKRANI

Natoa shukrani kwa Mungu kwa kunisaidia kufanikisha mafunzo yangu na kwa neema zake. Pia, ninamshukuru msimamizi wangu, Dkt. Wallace Kapele Mlaga, kwa msaada na mwongozo wake wa kitaalamu ambao umeniwezesha kukamilisha tasnifu hii kwa mafanikio.

Pia ninawashukuru mke wangu, Uwingeneye Marie Grace, na watoto wangu, Ngabo Cyusa Yvan na Gisa Jean de Dieu, kwa msaada wao mkubwa na upendo usio na kikomo. Shukrani zangu za dhati pia kwa wazazi wangu, Hategekimana Albert na Nyirantashya Marie Grace, pamoja na ndugu zangu wote ambao walijinyima mengi ili niweze kukamilisha safari yangu ya masomo. Mungu awabariki sana.

# TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabaruku kwa mke wangu, Uwingeneye Marie Grace, na watoto wangu, Ngabo Cyusa Yvan na Gisa Jean de Dieu. Upendo na msaada wao usio na kikomo umekuwa nguzo muhimu katika safari yangu ya masomo. Bila wao, nisingeweza kukamilisha tasnifu hii kwa mafanikio.

## IKISIRI

Utafiti wetu ulilenga kuchunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, malengo mahususi ya utafiti yalikuwa mawili. Mosi, kubainisha athari za kifonolojia za lugha ya Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera, Rwanda. Pili, kubainisha mikakati ya kukabili athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi. Wango la utafiti lilikuwa walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Sampuli ya utafiti ilikuwa walimu wa Kiswahili 7 na wanafunzi 76 ambao walichaguliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa. Mbinu za uchambuzi matini, ushuhudiaji na mahojiano zilitumika kukusanya data za kitaamuli ambazo zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa madondoo na maelezo. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa, kuna athari za kifonolojia katika ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Athari hizo ni pamoja na uchopekaji, udondoshaji, ubadilishaji wa fonimu na mpangilio mbaya wa mofimu katika maneno. Vilevile, matokeo yamebainisha sababu za athari hizo. Sababu ya kwanza ni ukosefu wa mafunzo ya kina ya fonetiki na fonolojia kwa wanafunzi. Pili, ni mazingira ya nyumbani na shuleni ambapo Kinyarwanda kinatumika zaidi kuliko Kiswahili.Tatu, ni shule kutilia mkazo zaidi ufundishaji wa sarufi na fasihi kuliko fonolojia. Isitoshe, matokeo ya utafiti yamebainisha mikakati ya kukabili athari hizo. Mikakati iliyotolewa ni pamoja na kulinganisha fonolojia ya Kinyarwanda na ya Kiswahili, kutoa mazoezi ya kutosha yanayohusiana na fonolojia ya Kiswahili na kuanzisha klabu za Kiswahili katika shule. Kwa hivyo, utafiti ulipendekeza ushirikiano baina ya wanafunzi, walimu na viongozi wa shule ili kuondoa athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

**Maneno ya Msingi:** *Fonolojia, Athari za Kifonolojia na Ujifunzaji wa Kiswahili*

## YALIYOMO

IKIRARI NA HAKIMILIKI ........ ii

ITHIBATI YA MSIMAMIZI ........ iii

SHUKRANI ........ iv

TABARUKU ........ v

IKISIRI ........ vi

YALIYOMO ........ vii

ORODHA YA VIFUPISHO ........ xii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ........ 1

1.0 Utangulizi ........ 1

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 1

1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti ........ 4

1.3 Malengo ya Utafiti ........ 5

1.3.1 Lengo la Jumla ........ 5

1.3.2 Malengo Mahususi ........ 5

1.4 Maswali ya Utafiti ........ 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 5

1.6 Mawanda ya Utafiti ........ 6

1.6.1 Mawanda ya Kimaudhui ........ 6

1.6.2 Mawanda ya Kimuda ........ 6

1.6.3 Mawanda ya Kijiografia ........ 7

1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wake ........ 7
1.8 Mpangilio Ripoti ya Utafiti ........ 8
1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ........ 8
SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO ........ 9
2.0 Utangulizi ........ 9
2.1 Dhana ya Fonolojia ........ 9
2.2 Dhana ya Fonimu ........ 10
2.2.1 Fonimu za Kiswahili na Kinyarwanda ........ 10
2.3Vipengele vya Fonolojia ........ 15
3.1 Kiimbo na Kidatu ........ 15
2.3.2 Mkazo ........ 17
2.3.3 Lafudhi ........ 18
2.3.4 Toni ........ 19
2.3.5 Mfuatano wa Sauti Kuunda Silabi ........ 20
2.3.6 Otografia ya Kiswahili na Kinyarwanda ........ 21
2.4 Athari za Kifonolojia za Lugha za Kibantu katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili ...... 23
2.5 Mikakati ya Kuondoa Athari za Kifonolojia za Kibantu katika Ujifunzaji wa Kiswahili .. 25
2.7 Mapengo ya Utafiti ........ 28
2.8 Kiunzi cha Nadharia ........ 29
2.9 Muhtasari wa Sura ya Pili ........ 30
SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI ........ 31
3.1 Utangulizi ........ 31

3.1 Paradima ya Utafiti ........................................................................................ 31
3.2 Usanifu wa Utafiti ........................................................................................ 32
3.3 Eneo la Utafiti ........................................................................................ 32
3.4 Wango na Sampuli ya Utafiti ........................................................................................ 33
3.4.1 Wango la Utafiti ........................................................................................ 33
3.4.2 Sampuli ya Utafiti ........................................................................................ 33
3.5 Mbinu za Kukusanyia Data ........................................................................................ 34
3.5.1 Uchanganuzi wa Matini ........................................................................................ 34
3.5.2 Usaili ........................................................................................ 35
3.5.3 Ushuhudiaji ........................................................................................ 35
3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa ........................................................................................ 36
3.6.1 Data za Msingi ........................................................................................ 36
3.6.2 Data za Upili ........................................................................................ 36
3.7 Vifaa vya Utafiti ........................................................................................ 36
3.8 Uchanganuzi wa Data ........................................................................................ 37
3.9 Itikeli za Utafiti ........................................................................................ 37
3.10 Uhalali na Uthabiti wa Utafiti ........................................................................................ 37
3.11 Muhtasari wa Sura ya Tatu ........................................................................................ 38
SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI .................. 39
4.0 Utangulizi ........................................................................................ 39
4.1 Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Ujifunzaji wa Kiswahili ............................ 39
4.1.1 Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Irabu .................................................. 39

4.1.1.1 Uchopekaji wa Irabu ........................................................................................ 40
4.1.1.2 Udondoshaji wa Irabu ...................................................................................... 42
4.1.1.3 Ubadilishaji wa Irabu ........................................................................................ 44
4.2 Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Konsonanti ............................................ 46
4.2.1 Athari ya Uchopekaji wa Konsonanti ..................................................................... 46
4.2.2 Athari ya Udondoshaji wa Konsonanti .................................................................... 48
4.2.3 Athari ya Ubadilishaji wa Konsonanti ..................................................................... 51
4.23 Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Mpangilio Mbaya wa Fonimu .............. 55
4.3 Mikakati ya Kukabili Athari ya Kifonolojia katika Kujifunza Kiswahili ........................... 58
4.3.1 Kulinganisha Fonolojia ya Kinyarwanda na ya Kiswahili .......................................... 59
4.3.2 Mazoezi ya Kutosha Yanayohusiana na Fonolojia ya Kiswahili ................................ 60
4.3.3 Kuanzisha Klabu za Kiswahili katika Shule ............................................................. 63
4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne ........................................................................................ 64
SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................................... 65
5.1 Utangulizi ................................................................................................................ 65
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ............................................................................... 65
5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza ..................................................................................... 65
5.2.2 Lengo Mahususi la Pili ............................................................................................ 65
5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti iliyotumika ................................................................. 66
5.4 Mapendekezo ........................................................................................................... 67
5.4.1 Mapendekezo kwa Walimu ..................................................................................... 67
5.4.2 Mapendekezo kwa Wanafunzi ................................................................................. 67

5.4.3 Mapendekezo kwa Viongozi wa Shule ........................................................ 67

5.4.4 Mapendekezo ya Tafiti Fuatizi ........................................................ 67

5.6 Muhtasari wa Sura ya Tano ........................................................ 68

MAREJELEO ........................................................ 69

VIAMBATISHO ........................................................ 74

# ORODHA YA VIFUPISHO

**Bw.**: Bwana

**Dkt.:** Daktari

**ES.:** Ecole Secondaire

**GS**: Groupe Scholaire

**khj**: Keshatajwa hapo juu

**MINEDUC**: Ministry of Education (Wizara ya Elimu)

**TEHAMA** : Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**whj**: Wameshatajwa hapo juu

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Sura ya kwanza ya tasnifu hii inajumuisha utangulizi kuhusu sura hii. Hivyo, inazingatia vipengele vifuatavyo: utangulizi, usuli wa utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti, mpangilio wa ripoti ya utafiti, na muhtasari wa sura ya kwanza.

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Lugha ni chombo muhimu katika mawasiliano na ujifunzaji wa binadamu. Bila kujali hisia zao, watu mara nyingi huvutiwa na kujifunza lugha ya piliili kuongeza ustadi wao wa mawasiliano. Hivyo, hupanua ufahamu wao wa tamaduni tofauti (Amara, 2015).Mchakato huu wa kujifunza lugha ya pili huchochea maendeleo ya kibinafsi na kiakili, na wakati mwingine hufungua milango ya fursa za kielimu na kikazi. Kwa hiyo, kujifunza lugha ya pili ni njia muhimu ya kuboresha uhusiano wa kibinadamu na kuchangia kwenye ujenzi wa dunia yenye uelewa na amani.

Ni kweli kwamba kujifunza lugha ya pili kunaweza kuathiriwa na lugha ya kwanza. Athari hizi zinaweza kujitokeza katika viwango tofauti vya lugha ambazo ni sauti, maneno, tungo na maana. (Gekondo, 2019). Athari hizi mara nyingi zinatokana na kwamba wajifunzaji lugha wanakosa uelewa wa kina wa kanuni za lugha mpya.

Wao wanashindwa kutafsiri kanuni za lugha yao ya kwanza kwa lugha wanayojifunza, hali inayoweza kupelekea kufanya makosa.. Hata hivyo, kuelewa na kutambua athari hizi ni hatua muhimu katika kuboresha mchakato wa kujifunza lugha ya pili na kuwezesha mafanikio bora kwa wanafunzi.

Munyua (2002) anaelezea kwamba lugha ya kwanza inaweza kuwa na athari mbaya kwa ujifunzaji wa lugha ya pili. Hii inatokea pale ambapo mwanafunzi huhamisha vipengele vya lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Hali hii inaweza kuwa kikwazo kwa mwanafunzi katika umahiri wa lugha ya pili, kwa sababu anatumia mara kwa mara miundo ya lugha ya kwanza katika muktadha wa lugha ya pili.

Maelezo ya Munyua (khj) yanatoa mwanga kuhusu jinsi uhamishaji wa vipengele vya lugha ya kwanza unaweza kuzuia mafanikio katika kujifunza lugha ya pili. Hoja hii ilituchochea kufanya utafiti ili tuchunguze jinsi uhamishaji wa vipengele vya kifonolojia vya Kinyarwanda unavyoweza kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

Masebo na Nyangwine (2008) wanadai kwamba ujifunzaji wa Kiswahili unaweza kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na lugha za Kibantu, ambazo ni kwanza kwa baadhi ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Lugha za Kibantu, kama vile Kiolusuba (Otiende, 2013), Kijita (Wenceslaus, 2015), Kinyamwezi (Nyanda, 2018), na Kisamia (Wanjala, Mukoyani & Agaba, 2023), zinaweza kuwa na athari katika muundo wa sentensi, sarufi na matamshi ya wanafunzi wanapojifunza Kiswahili.

Masebo na Nyangwine (whj) wanaendelea kusema kwamba, lugha ya kwanza ya mwanafunzi, hasa ya Kibantu, inaweza kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Athari hizi hutokana na kufanana kwa vipengele vya kimuundo na kisarufi kati ya Kiswahili na lugha hizo. Hivyo, wanafunzi hujaribu kutumia kanuni za lugha yao ya kwanza, kama vile mfuatano wa maneno, viambishi na msamiati wanapotumia lugha ya pili. , Jambo linaloweza kusababisha makosa na kupunguza ufanisi wa ujifunzaji.

Ndiyo sababu, utafiti uliofanyika ulichunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili, kwa lengo la kuboresha mbinu za ufundishaji wa Kiswahili ambazo zinatumiwa katika shule za seondari teule wilayani Bugesera.

Zaidi ya hayo, utafiti wa Otiende (2013) ulishughulikia athari za kifonolojia za Kiolusuba katika ujifunzaji wa Kiswahili. Utafiti wake unasisitiza kwamba asilimia 65 ya maneno katika lugha ya Kiswahili yanafanana na maneno kutoka lugha za asili za Kibantu. Hii inaonesha kiwango kikubwa cha ulinganifu wa kileksimu kati ya Kiswahili na lugha za Kibantu. Vilevile, Nyanda (2015) anaeleza kwamba ni jambo la kawaida kuona kwamba ujifunzaji wa Kiswahili unaweza kuathiriwa na lugha hizi, hasa kwa makabila yanayotumia Kiswahili kama lugha ya pili. Maelezo haya yanatoa mwangaza kuhusu jinsi lugha za asili ya Kibantu zinavyoweza kuwa na athari kubwa katika ujifunzaji wa Kiswahili.

Hivyo basi, athari za lugha ya kwanza kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili zinaonekana wazi katika tafiti mbalimbali. Mangi (2019) anabainisha kwamba wanafunzi wa Kiswahili kutoka jamii ya Watanzania wanaotumia Kinyaturu wanakumbana na changamoto kubwa katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili kutokana na athari za lahaja yao.

Athari hizi hujitokeza kwenye mofolojia, kama vile matumizi ya viambishi vya nomino na vitenzi, pamoja na sintaksia, ambapo mfuatano wa maneno na uundaji wa sentensi huathiriwa na kanuni za Kinyaturu. Athari hizi zinaweza kusababisha makosa katika matumizi sahihi ya Kiswahili na kupunguza ufanisi wa ujifunzaji. Hali hii ilituchochea kufanya utafiti wetu ili tuchunguze ikiwa Kinyarwanda ni mojawapo ya lugha za Kibantu ambazo zinaweza kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili. Utafiti wetu ulilenga kuchunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili, kwa kuwa fonolojia huchukuliwa kama kitovu cha ujifunzaji lugha yoyote (Ndungu, 1999).

Athari za kifonolojia ni mabadiliko yanayotokea katika matamshi ya lugha ya pili kutokana na ushawishi wa lugha ya kwanza. Hata yanaweza kusababisha tofauti katika lafudhi, sauti za maneno, na ufasaha wa wanafunzi wanapojifunza lugha mpya kama Kiswahili (Wanjala, Mukoyani, & Agaba, 2023).

Kwa mujibu wa Manundu (2019), wanafunzi wa Kiswahili nchini Somalia wanakumbwa na changamoto za kimofolojia kutokana na athari za lugha ya Kisomali, kama vile kutofautiana kwa uundaji wa viambishi na vitenzi. Vilevile, Bizimana (2022) anaeleza changamoto zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili nchini Burundi. Changamoto hizi zinatokana na athari za mofolojia ya Kirundi, hususan kwenye uundaji wa maneno na viambishiKwa upande wa fonolojia, Ontieri (2010) anabainisha jinsi lugha za Kibantu zinazotumiwa nchini Kenya zinavyoathiri uwezo wa wanafunzi kutamka maneno kwa usahihi katika Kiswahili.

Wanjala, Mukoyani na Agaba (2023) wanasisitiza kuwa athari za kifonolojia za lugha ya kwanza, kama vile tofauti za matamshi na lafudhi, zinakwamisha ufasaha wa wanafunzi wa Kiswahili nchini Uganda. Kwa ujumla, tafiti hizi zinaonesha athari maalum kama vile tofauti za mofolojia na fonolojia zinavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika maeneo mbalimbali, na hivyo kuleta changamoto kwa ufanisi wa ujifunzaji wa lugha hii.

Isitoshe, lugha ya Kinyarwanda inaathiri ujifunzaji wa Kiswahili nchini Rwanda kwa njia kadhaa. Kwanza, tofauti za matamshi husababisha wanafunzi kutamka maneno ya Kiswahili kwa lafudhi ya Kinyarwanda, hivyo kupunguza ufasaha wao. Pili, muundo wa sentensi wa Kinyarwanda huathiri sarufi ya Kiswahili. Tatu, utofauti wa msamiati huchangia katika makosa ya matumizi ya maneno. Mwisho, mfuatano wa sauti wa Kinyarwanda huleta ugumu kwa wanafunzi kufuata mfuatano sahihi wa silabi katika Kiswahili (Kimenyi, 2003; Ntawiyanga, 2015; Niyomugabo, 2016; Mukashyaka, 2023). Hivyo basi, tulihamasishwa kufanya utafiti ili kuchunguza kwa undani athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera nchini Rwanda.

### 1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Changamoto katika ujifunzaji wa lugha ya pilimara nyingi hutokana na kutoelewa vizuri kanuni za lugha hiyo. Hii inatokana na kwamba lugha ya kwanza huathiri lugha ya pili katika viwango vya sauti(kifonolojia), meneno (kimofolojia) tungo,(kisintaksia) na maana, (kisemantiki). (Gekondo, 2019). Kwa mujibu wa Masebo na Nyangwine (2008), ujifunzaji wa Kiswahili hasa huathiriwa na lugha za Kibantu ambazo ni lugha za kwanza kwa baadhi ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Hivyo, lugha hizi zinaweza kuwa na athari katika muundo wa sentensi, sarufi na matamshi ya wanafunzi wanapojifunza Kiswahili.

Kwa upande mwingine, Kimenyi (2013), Ntawiyanga (2015), Niyomugabo (2016), na Mukashyaka (2023) wameonesha kuwa Kinyarwanda kinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili nchini Rwanda. Hivyo wanafunzi wanafanya makosa katika matumizi ya maneno ya Kiswahili katika mawasiliano yao.

Hivyo basi, tuliamua kufanya utafiti wetu ili kuchunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera . Hii inatokana na hoja kwamba fonolojia inachangia katika ujifunzaji wa lugha yoyote. Bila kuelewa athari za kifonolojia kwa undani, wanafunzi wanaweza kuendelea kukabiliana na changamoto za matamshi, lafudhi na ufasaha wa Kiswahili, hali inayoweza kudhoofisha uwezo wao wa kujieleza kwa usahihi katika Kiswahili. Hivyo, utafiti unatarajiwa kutoa maarifa yatakayosaidia kuboresha mbinu za ufundishaji wa Kiswahili na kusaidia wanafunzi kukabiliana na changamoto

zinazotokana na athari za Kinyarwanda, hivyo kuongeza ufanisi wa ujifunzaji na utumizi wa lugha hiyo

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti wetu yanagawanyika katika lengo la jumla na malengo mahususi.

#### 1.3.1 Lengo la Jumla

Lengo la jumla lilikuwa kuchunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

#### 1.3.2 Malengo Mahususi

i) Kubainisha athari za kifonolojia za lugha ya Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera;

ii) Kupendekeza mikakati ya kukabili athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

i) Je, ni athari gani za kifonolojia za lugha ya Kinyarwanda zinazoathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera?

ii) Ni mikakati gani inayoweza kutumiwa ili kukabili athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti yatakuwa na umuhimu mkubwa kwa walimu wa Kiswahili, wanafunzi wa Kiswahili, Bodi ya Elimu ya Msingi ya Rwanda na wapangaji wa elimu. Kwanza, matokeo ya utafiti huu yatatoa mwangaza muhimu kwa walimu wa Kiswahili kuhusu jinsi athari za Kinyarwanda zinavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi. Walimu watapata maarifa ya kuboresha mbinu zao za ufundishaji kwa kuzingatia changamoto zinazotokana na athari za lugha ya kwanza. Hii itawawezesha kuunda mikakati bora na kuweka mkazo kwenye maeneo yenye changamoto kubwa, hivyo kuboresha ufanisi wa ufundishaji wa Kiswahili.Pili, wanafunzi wa Kiswahili watapata manufaa makubwa kutokana na utafiti huu. Uelewa wa kina wa athari za

Kinyarwanda katika kujifunza Kiswahili utawawezesha wanafunzi kuelewa kwa urahisi namna ya kuepuka makosa yanayotokana na tofauti za kifonolojia na kuboresha mchakato wao wa ujifunzaji. Hii itasaidia katika kuimarisha ufasaha wao wa lugha ya Kiswahili na kuwapatia ujasiri wa kushiriki kikamilifu katika masomo yao. Kwa hiyo, wanafunzi watanufaika kwa kuwa na mazingira bora ya kujifunza, ambayo yataboresha stadi zao katika Kiswahili na kuongeza ufanisi wao katika matumizi ya lugha hiyo.

Tatu, Bodi ya Elimu ya Msingi ya Rwanda itakuwa na jukumu muhimu katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na utafiti huu. Taarifa zitakazopatikana zitatoa mwangaza kwa bodi hiyo kuhusu mabadiliko yanayohitajika katika mitaala ili kujumuisha mahitaji ya wanafunzi wanaokumbwa na athari za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili. Hii itatoa mwongozo wa kimkakati katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili, pamoja na kuimarisha misingi ya ufundishaji Kwenye nchi ya Rwanda.

Mwisho, wapangaji wa elimu watapata taarifa muhimu kutoka kwa utafiti huu ambazo zitawasaidia katika kutengeneza miongozo bora ya ufundishaji wa Kiswahili Kwenye nchi ya Rwanda. Kwa kuzingatia matokeo haya, wapangaji wa elimu wanaweza kubuni sera na mikakati itakayosaidia kuziba mapengo yaliyopo katika mchakato wa ujifunzaji.

Hii itahakikisha kuwa walimu wanapata msaada unaofaa na rasilimali za kutosha ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

## 1.6 Mawanda ya Utafiti

Mawanda ya utafiti ulihusisha mawanda matatu.

### 1.6.1 Mawanda ya Kimaudhui

Kulingana na mada ya utafiti wetu, kwa upande wa maudhui.utafiti wetu ulijikita kwenye athari za kifonolojia za Kinyarwanda tu ambazo zinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

### 1.6.2 Mawanda ya Kimuda

Kwa upande wa muda, utafiti ulihusisha mwaka wa 2023 na 2004. Utafiti ulifanyika katika kipindi cha miaka miwili tu ili kupata data za kuaminika kuhusu athari za kifonolojia za

Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.Uchaguzi wa miaka miwili unalenga kuchunguza mabadiliko ya muda mfupi na kuthibitisha mwelekeo wa sasa katika athari hizi.

### 1.6.3 Mawanda ya Kijiografia

Kwa upande wa jiografia, utafiti ulifanyika katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Shule hizo ni pamoja na: GS Nyiragiseke, Kamabuye, Nyirarukobwa na GS Kagasa Mwogo. Shule ya sekondari ya Nyiragiseke na Kamabuye ni shule ambazo zinakaribiana na mpaka wa Rwanda na Burundi ambapo panaishi watu wanaozungumza Kiswahili. Aidha, shule ya sekondari ya Nyirarukobwa na Kagasa Mwogo ni shule za wilaya ya Bugesera ambazo zinakaribiana na mji wa Kigali ambapo kuna idadi kubwa ya watu wanaozungumza Kiswahili.

Wilaya ya Bugesera ilichaguliwa kwa utafiti huu kutokana na nafasi yake ya kijiografia na kitamaduni. Inapakana na Burundi, ambako Kiswahili kinatumika sana, na pia iko karibu na mji wa Kigali, kitovu cha biashara na shughuli za kimataifa, hivyo shule zake zina ushawishi mkubwa wa lugha ya Kiswahili. Ukaribu na mipaka ya Burundi na Kigali unaleta fursa ya kipekee ya kuchunguza ujifunzaji wa Kiswahili na athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika shule za sekondari wilayani Bugesera.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wake

Wakati wa kufanya utafiti, mtafiti alikabiliwa na vikwazo tofauti. Kwanza, mtafiti alichelewa kupata kibali kutoka Kurugenzi ya Utafiti na Ubunifu ya Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu, kwa sababu mkurugenzi alikuwa katika likizo. Ili kukabiliana na kikwazo hiki, mtafiti alitafuta taarifa kuhusu tarehe ya kurudi kazini ya mkurugenzi huku akiendelea kutayarisha nyenzo zake za utafiti. Mbinu hii ilimsaidia kuokoa muda na kuwa na maandalizi mazuri ili kuendelea na mchakato wa utafiti mara tu kibali kilipopatikana

Pili, kwa kuwa utafiti ulifanyiwa kwenye shule ambazo hazikaribiani. Ili kukabiliana na kiwazo, cha kufika katika kila shule. Mtafiti alifanya ratiba maalum ya kutembelea kila shule. Hivyo, kila shule ilitengewa siku yake. Mbinu hii ilizaa matunda, kwani mtafiti alifanikiwa kufikia kila shule na kukamilisha ukusanyaji

## 1.8 Mpangilio Ripoti ya Utafiti

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza inajumuisha utangulizi. Sura ya pili inahusu mapitio ya maandiko. Sura ya tatu inajadili mbinu za utafiti. Sura ya nne inazingatia uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Sura ya tano ni muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho, na mapendekezo ya utafiti.

## 1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura ya kwanza ya utafiti inatoa utangulizi kuhusu utafiti uliofanyika. Sura hii inashughulikia vipengele vifuatavyo: utangulizi, usuli wa utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti, mpangilio ripoti ya utafiti, na muhtasari wa sura ya kwanza.

# SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.0 Utangulizi

Sura ya pili inahusu mapitio ya maandiko yanayohusiana na mada ya utafiti wetu. .Sura hii inagawanyika katika sehemu zifuatazo: utangulizi, dhana ya fonilojia, dhana ya fonimu, vipengele vya fonolojia, athari kifonolojia za lugha za Kibantu katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na mikakati ya kuondoa athari za kifonolojia Kibantu katika ujifunzaji wa Kiswahili. Aidha, sehemu hii inahusisha, mapengo ya utafiti, kiunzi cha nadharia na muhtasari.

## 2.1 Dhana ya Fonolojia

Fonolojia ni tawi la isimu ambalo linachunguza jinsi sauti za lugha zinavyofanya kazi na kutumika katika lugha mbalimbali (Habwe & Karanja, 2004).Tawi hili linajikita zaidi katika kuchunguza jinsi sauti zinavyopangika, kuunganishwa, na kutumika kuunda tungo zenye maana katika lugha fulani. Hivyo, utafiti wa fonolojia katika lugha kama vile Kinyarwanda unalenga kuelewa namna sauti zinavyotumika na mpangilio wake katika lugha hiyo. Fonolojia inaangazia kanuni na sheria zinazohusiana na utamkaji na matumizi ya sauti zinazosaidia kupambanua maana katika lugha husika.

Kwa mujibu wa Massamba (2004), fonolojia ni tawi la isimu linalochunguza mfumo na ruwaza za sauti katika lugha maalum ya binadamu. Hii inamaanisha kuwa fonolojia inaangalia jinsi sauti zinavyopangika na kutofautisha maana ndani ya lugha fulani. Kwa hiyo, ni muhimu kufanya utafiti wa kina katika fonolojia ya lugha kama Kiswahili ili kuelewa kanuni zinazoongoza utumiaji wa sauti zake. Sheria hizi ndizo zinazowezesha utoaji sahihi wa sauti, ambazo ni muhimu katika kupambanua maana ya tungo katika lugha.

Fonolojia inajikita hasa katika sauti ambazo zina uwezo wa kubadilisha maana ya neno au tungo katika lugha fulani. Hivyo, uchambuzi wa fonolojia ya Kiswahili na Kinyarwanda unalenga kuchunguza jinsi sauti za lugha hizo zinavyotumika na kuathiriana. Kwa mfano, utafiti unaweza kufuatilia tofauti za kifonolojia kati ya lugha hizo mbili na jinsi athari za sauti za Kinyarwanda zinavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili.

Utafiti wetu ulikuwa na lengo la kuchunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa sekondari katika wilaya ya Bugesera, Rwanda. Uchunguzi huu ulitarajia kutoa mwanga juu ya athari za kifonolojia ambazo wanafunzi wa Kinyarwanda hukutana nazo wanapojifunza Kiswahili na jinsi zinavyoathiri uwezo wao wa kupata umahiri wa lugha hiyo. Matokeo ya utafiti huu yalitarajiwa kusaidia kuboresha mbinu za kufundisha lugha kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

### 2.2 Dhana ya Fonimu

Fonimu ni kipashio kidogo zaidi cha fonolojia kinachoweza kubadili maana ya neno (Njogu na wenzake, 2006). Kwa mfano, mwanafunzi msemaji wa Kinyarwanda anaposema neno “papa” badala ya “baba”, tofauti ya sauti /p/ na /b/ huleta mabadiliko ya maana. Kwa hivyo, sauti ya /p/ ni fonimu katika Kiswahili kwa sababu inabadilisha maana ya neno. Massamba na wenzake (2004), wanaunga mkono kauli hii kwa kusema kuwa fonimu ni vitamkwa vinavyobadilisha au kuunda maneno yenye maana tofauti. Aidha, Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa fonimu ni kipashio kidogo zaidi kinachobainisha maana katika lugha. Kwa mfano, katika Kiswahili, maneno “saa” na “taa” yanatofautiana kwa sauti moja tu, ambayo ni /s/ na /t/, na hivyo sauti hizo ni fonimu kwa sababu zinatofautisha maana.

Kwa mujibu wa Mgullu (2001), ni muhimu kuelewa fonimu za lugha pamoja na sifa zake ili kuzitumia ipasavyo. Fonimu ina sifa za kifonetiki na kifonolojia, na wasemaji wa lugha wanapaswa kuelewa sifa hizi kama sehemu ya umilisi wao wa lugha. Fonimu hushiriki katika kujenga na kutofautisha maana ya neno. Aidha, mabadiliko yoyote ya fonimu, kama kubadilisha, kuongeza au kupunguza, yanaweza kubadili kabisa maana ya neno. Kwa mfano, kubadili sauti /s/ na /k/ katika neno “sali” kunaleta neno “kali” lenye maana tofauti (Mgullu, khj). Kwa hiyo, uelewa wa fonimu za Kiswahili na Kinyarwanda ni muhimu ili kuchunguza uhusiano wa kifonolojia na jinsi athari za Kinyarwanda zinavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi.

#### 2.2.1 Fonimu za Kiswahili na Kinyarwanda

Kiswahili na Kinyarwanda ni lugha za kibantu ambazo zina alifabeti zinszogawanyika katika makundi matatu yafuatayo:

Mosi ni Irabu. Manundu (2019) anaeleza kuwa irabu ni vitamkwa vinavyotolewa bila kizuizi katika mkondo wa hewa unaotoka mapafuni kupitia kinywa na pua. Aidha, irabu hutamkwa bila ala za kutamkia kukaribiana kiasi cha kuzuia au kukatiza hewa, tofauti na konsonanti. Lugha ya Kiswahili ina irabu tano. Vilevile, Ndihokubwayo (2003) anasema kwamba Kinyarwanda kina irabu tano. Mfano ufuatao unaeleza.

| **Irabu za Kiswahili** | | **Irabu za Kinyarwanda** | |
|---|---|---|---|
| **Maandishi ya Mawaida** | **Unukuzi wa Fonimu** | **Maandishi ya Mawaida** | **Unukuzi wa Fonimu** |
| /a/ | /a/ | /a/ | /a/ |
| /e/ | /Ɛ/ | /e/ | /Ɛ/ |
| /i/ | /i/ | /i/ | /i/ |
| /o/ | /ɔ/ | /o/ | /ɔ/ |
| /u/ | /u/ | /u/ | /u/ |

Kulingana na Manundu (2019), Kiswahili kina fonimu tano za irabu ambazo zina namna ya kawaida ya kuandikwa na pia unukuzi wake wa kifonimu. Irabu /a/, /e/, /i/, /o/, na /u/ zinawakilishwa kama /a/, /Ɛ/, /i/, /ɔ/, na /u/ katika unukuzi wa kifonimu mtawalia. Kwa mfano, irabu "e" kawaida huandikwa kama /e/, lakini kifonetiki inanakiliwa kama /Ɛ/ kwa sababu sauti hiyo ni pana zaidi katika matamshi halisi.

Aidha, Ndihokubwayo (khj) anaonesha kwamba Kinyarwanda kinazo irabu tano ambazo zinanukuliwa kama /a/, /Ɛ/, /i/, /ɔ/, na /u/. Hii inaonesha kwamba fonimu za irabu za Kiswahili ni sawa na fonimu za Kinyarwanda. Kwa mujibu wa Massamba, Kihore na Hokororo (2009), ulinganifu huu wa fonimu za irabu kati ya Kiswahili na lugha za kibantu unaonesha kuwa kuna mfanano wa kifonolojia baina ya lugha hizi, ingawa zinaweza kuwa na tofauti nyingine katika matamshi na matumizi.

Mjadala kuhusu utamkaji wa vokali katika Kiswahili, kama ulivyojadiliwa na Polomé (khj) na Clark & Yallop (1990), unaonesha kuwa vokali kama /e/ na /o/ zinaweza kubadilika kulingana na

muktadha wa kimatamshi, zikitamkwa kama [e] au [ɪ] na [o] au [ʊ], mtawalia. Tofauti na Kiswahili, irabu za Kinyarwanda zina sifa za kipekee za kisikizi ambazo huathiri moja kwa moja maana ya maneno, kama inavyobainishwa na Ndihokubwayo (khj).

Kwa mfano, irabu ya /a/ katika neno "abana" (watoto) na /e/ katika "emera" (kubali) zina sifa tofauti zinazoleta maana tofauti. Aidha, Kinyarwanda haliruhusu kufuatana kwa irabu mbili, isipokuwa katika matumizi maalum kama vile kuonesha saa (Inteko Nyarwanda y' Ururimi n' Umuco, 2014), tofauti na Kiswahili. Sifa hizi za kipekee huchangia utajiri na uchangamano wa lugha ya Kinyarwanda.

Manundu (2019) anasema kwamba ni jambo la kawaida kwamba ujifunzaji wa Kiswahili unaweza kuathiriwa na athari za kifonolojia za mojawapo wa lugha za Kibantu Hivyo basi, tumeamua kufanya utafiti wetu ili tuone kwamba kuna athari zozote za kifonolojia za irabu za Kinyarwanda ambazo zinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Bugesera nchini Rwanda. Pia, utafiti wetu ulitarajia kutoa mbinu mwafaka zo kuepukana na athari hizo.

Pili ni KonsonantiKwa mujibu wa Massamba (2004), konsonanti ni aina ya fonimu zinazozuiliwa kwa kiasi fulani au kikamilifu wakati wa kutamkwa, kwa kizuizi chochote katika mkondo wa hewa. Katika Kiswahili, kuna jumla ya konsonanti ishirini na tano (25) ambazo hutumika kutengeneza maneno na sentensi. Aidha, kulingana na Ndihokubwayo (khj), Kinyarwanda kina jumla ya konsonanti ishirini na mbili (22) ambazo pia zina jukumu muhimu katika uundaji wa maneno na sentensi katika lugha hiyo. Ufuatao ni uandishi wa kawaida na unukuzi wa fonimu za konsonanti kwa Kiswahili kama inavyobainishwa na Polomé (1967) na za Kinyarwanda kama inavyopendekezwa na Ndihokubwayo (khj).

| **Konsonanti za Kiswahili** | | **Konsonanti za Kinyarwanda** | |
|---|---|---|---|
| **Maandishi ya Mawaida** | **Unukuzi wa Fonimu** | **Maandishi ya Mawaida** | **Unukuzi wa Fonimu** |
| /b/ | /b/ | /b/ | /b/ |
| /ch/ | /ʧ/ | /c/ | /ʧ/ |
| /d/ | /d | /d/ | /d |
| /dh/ | /ð/ | - | - |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /f/ | /f/ | /f/ | /f/ |
| /g/ | /g/ | /g/ | /g/ |
| /gh/ | /ɣ/ | - | - |
| /h/ | /h/ | /h/ | /h/ |
| /j/ | /J/ | /j/ | /J/ |
| /k/ | /k/ | /k/ | /k/ |
| /kh/ | /χ/ | - | - |
| /l/ | /l/ | /l/ | /l/ |
| /m/ | /m | /m/ | /m |
| /n/ | /n/ | /n/ | /n/ |
| /ng'/ | /ŋ/ | - | - |
| /ny/ | /ɲ] | - | - |
| /p/ | /p/ | /p/ | /p/ |
| /r/ | /r/ | /r/ | /r/ |
| /s/ | /s/ | /s/ | /s/ |
| /sh/ | / ʃ/ | - | - |
| /t/ | /t/ | /t/ | /t/ |
| /th/ | /Ө/ | - | - |
| /v/ | /v/ | /v/ | /v/ |
| /z/ | /z/ | | /z/ |

Konsonanti katika lugha ya Kiswahili zina sifa muhimu ambazo zinaathiri utamkaji na ufahamu wa sauti mbalimbali. Kama alivyobainisha Kipacha (2007), sauti za konsonanti kama vile /p/, /b/, na /m/ zinahitaji midomo kukutanisha, na hivyo hujulikana kama sauti za mdomo. Aidha, sauti kama /f/ na /v/ zinahitaji kugusana kwa meno ya juu na mdomo wa chini, zikijulikana kama sauti za mdomo-meno.

Aidha, konsonanti kama /ɵ/ na /ð/ zinahitaji ncha ya ulimi kugusana na meno ya juu, nazo sauti za ufizi kama /t/, /d/, na /n/ zinahusisha ncha ya ulimi kugusana na ufizi wa juu. Sauti za kaakaa

gumu, kama /ʧ/ na /ʃ/, zinahitaji sehemu ya nyuma ya ulimi kugusana na kaakaa gumu, ilhali sauti za kaakaa laini kama /k/ na /g/ zinahusisha sehemu hiyo kugusana na kaakaa laini. Kwa kuongeza, sauti za glota kama /h/ zinahusisha kukutanisha nyuzi sauti kwa muda mfupi ili kutoa sauti maalum. Kulingana na Kihore, Massamba, na Msanjila (2003), sifa hizi za konsonanti ni muhimu kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili ili kufanikisha utamkaji wa sauti kwa usahihi.

Kwa upande wa Kinyarwanda, fonolojia yake inajumuisha konsonanti 21 ambazo zina sifa za kipekee za utamkaji na kisikizi. Kulingana na MINEDUC (2019), konsonanti hizi zimegawanywa katika makundi manne makuu. Kundi la kwanza ni la konsonanti za mdomo, ambazo hutamkwa kwa kutumia midomo, kama vile /b/, /p/, /f/, na /v/. Kundi la pili linajumuisha konsonanti za meno, ambazo hutamkwa kwa kutumia meno na ulimi, kama vile /d/, /t/, /s/, na /z/. Kundi la tatu linajumuisha konsonanti za koo kama /k/, /g/, /h/, na /ɲ/, ambazo hutamkwa kwa kutumia sehemu ya nyuma ya koo. Mfumo huu wa konsonanti katika Kinyarwanda unaonesha muundo rahisi wa sauti ikilinganishwa na Kiswahili, lakini kila konsonanti ina jukumu muhimu katika uundaji wa silabi na maneno.

Tofauti muhimu kati ya konsonanti za Kiswahili na Kinyarwanda ni kwamba Kiswahili kina konsonanti za ziada kama /dh/ (/ð/), /gh/ (/ɣ/), /kh/ (/χ/), /ng'/ (/ɧ/), /ny/ (/ɲ/), /sh/ (/ʃ/), na /th/ (/Ɵ/) ambazo hazipatikani katika Kinyarwanda. Kutokuwepo kwa konsonanti hizi katika Kinyarwanda kunaweza kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kinyarwanda, kwani wanaweza kuwa na changamoto ya kutamka au kutofautisha konsonanti hizo zisizokuwepo katika lugha yao ya kwanza. Hali hii inaweza kuhitaji mbinu maalum za kufundisha fonolojia ya Kiswahili ili kuwawezesha wanafunzi hao kutofautisha na kuzitumia konsonanti hizo kwa usahihi.

Kwa hiyo, tuliamua kufanya utafiti wetu ili tuchunguze ikiwa fonolojia ya Kinyarwanda inaweza kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Biugesera nchini Rwanda.

Aina ya tatu  ni Nusu-KonsonantiKwa mujibu wa wataalamu wa Massamba (2004), nusu-konsonanti ni fonimu ambazo zinakaa katikati ya konsonanti na irabu, na kwa Kiswahili, kunazo nusu-konsonanti mbili ambazo ni /w/ na /y/. Aidha, kulingana na MINEDUC (khj), hivi ni vitamkwa ambavyo vina sifa za kuwa kati ya konsonanti na irabu, hivyo huitwa nusu-konsonanti

au nusu-irabu. Katika lugha ya Kinyarwanda, nusu-konsonanti ni pamoja na /w/ na /y/, kama ilivyo katika Kiswahili. Ufuatao ni uandishi wa kawaida na unukuzi wa fonimu za nusu-konsonanti kwa Kiswahili na Kinyarwanda:

| **Nusu-Konsonanti za Kiswahili** | | **Nusu-Konsonanti za Kinyarwanda** | |
|---|---|---|---|
| **Maandishi ya Mawaida** | **Unukuzi wa Fonimu** | **Maandishi ya Mawaida** | **Unukuzi wa Fonimu** |
| /w/ | /w/ | /w/ | /w/ |
| /y/ | /j/ | /y/ | /j/ |

Kwa mujibu wa Massamba (2004), nusu-konsonanti ni fonimu zinazokaa katikati ya konsonanti na irabu, na katika Kiswahili, nusu-konsonanti hizi ni /w/ na /y/. Aidha, MINEDUC (khj) inathibitisha kuwa nusu-konsonanti hizi pia huitwa nusu-irabu kwa sababu zina sifa zinazochanganya pande zote mbili. Katika lugha ya Kinyarwanda, nusu-konsonanti hizi pia ni /w/ na /y/, ingawa fonimu ya /y/ hutamkwa kama /j/ katika unukuzi wa fonimu kwa lugha zote mbili. Hii inaonesha uhusiano wa karibu kati ya fonolojia ya Kiswahili na Kinyarwanda, jambo ambalo linaweza kusababisha mwingiliano katika ujifunzaji wa lugha hizi mbili. Kwa msingi huu, tumeamua kufanya utafiti wetu ili kuchunguza ikiwa fonimu za nusu-konsonanti zinaweza kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Bugesera, Rwanda.

### 2.3Vipengele vya Fonolojia

Fonolojia inahusisha vipengele tofauti ambavyo ni kiimbo na kidatu, mkazo, lafudhi, toni,uundaji wa silabi, na ortografia (Kihore, Massamba na Msanjila, 2003). Sehemu inayofuata inatoa maarifa zaidi kuhusu vipengele hivi.

### 3.1 Kiimbo na Kidatu

Kila lugha ya binadamu ina mpangilio wake wa kiimbo, ambao ni utaratibu wa kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa usemaji (Massamba, 2004). Kiimbo kinajumuisha mfuatano wa sauti, ambapo sauti zinaweza kupandishwa au kushushwa kulingana na muktadha. Kwa upande mwingine, kidatu kinahusiana na kiwango cha sauti kinachosikika wakati wa

utamkaji, kama vile kiwango cha juu, cha kati, au cha chini. Hivyo, tofauti kati ya kiimbo na kidatu inabainisha kuwa kiimbo linahusisha mabadiliko ya sauti, wakati kidatu kinahusiana na kiwango cha sauti kinachosikika (Massamba, khj).

Katika Kiswahili, kiimbo kina umuhimu mkubwa katika uelewa wa maneno na mitindo ya kusema. Kiswahili huweka mkazo kwenye silabi fulani, ambayo inasaidia kubaini maana ya maneno na kuathiri jinsi maneno yanavyotamkwa. Kwa mfano, Kiswahili kinajulikana kwa kuweka mkazo kwenye silabi ya pili kutoka mwisho, jambo ambalo linaweza kuathiri uelewa wa wasikilizaji (Masalu, 2019). Mabadiliko katika kiimbo yanaweza kuleta tofauti za maana, kama vile katika maneno yenye muktadha tofauti, ambayo yanahitaji wasemaji kuelewa jinsi ya kutamka kwa usahihi ili kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa.

Katika Kinyarwanda, kiimbo pia ni kipengele muhimu kinachohusiana na matamshi na sauti. Hapa, shadda (au kiimbo) inatumika kama njia ya kuonesha mabadiliko ya sauti na inaweza kubadilisha maana ya maneno (Niyonkuru, 2018). Kinyarwanda kina muundo wa kiimbo ambacho kinajumuisha kupandisha na kushusha sauti, lakini pia kinategemea shadda, ambayo inasaidia kubaini na kubadilisha maana. Hivyo, tofauti za kiimbo na matumizi ya shadda katika Kinyarwanda huchangia katika kueleweka na kutamkwa kwa maneno, na kuleta changamoto kwa wanafunzi wa Kiswahili wanaojifunza kutokana na Kinyarwanda.

Tofauti kati ya kiimbo katika Kiswahili na Kinyarwanda inajitokeza zaidi kutokana na kanuni zinazotawala matumizi ya sauti katika lugha hizi mbili. Katika Kiswahili, kiimbo kinahusishwa na msisitizo wa silabi, hasa silabi ya pili kutoka mwisho, jambo ambalo linaathiri maana na namna ya kutamka maneno. Kwa upande mwingine, Kinyarwanda kina mfumo wa kiimbo unaojumuisha vipengele vya kupanda na kushuka kwa sauti, lakini pia kinategemea zaidi matumizi ya shadda, yaani kurudia kwa silabi, ambayo inaweza kubadilisha kabisa maana ya neno (Niyonkuru, 2018).

Tofauti hizi katika mifumo ya kiimbo zinaweza kuwa changamoto kwa wanafunzi wa Kiswahili ambao lugha yao ya kwanza ni Kinyarwanda, kwani wanaweza kuchanganya msisitizo wa silabi au namna ya kutumia sauti katika Kiswahili kutokana na mwelekeo wa lugha yao ya asili. Hali hii imetupa shauku ya kufanya utafiti wetu ili tuchunguze jinsi kiimbo cha Kinyarwanda

kinavyoweza kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera nchini Rwanda.

### 2.3.2 Mkazo

Kila lugha ina utaratibu wake maalumu wa mpangilio wa sauti, ambapo mkazo unachukua nafasi muhimu. Mkazo ni dhana inayohusishwa na namna maneno au silabi zinavyotamkwa kwa nguvu tofauti. Halliday (1970) anaeleza mkazo kama hali ya kulitamka neno au silabi fulani kwa nguvu zaidi kuliko silabi nyingine, hivyo kuifanya husikike kwa urahisi na kuwa na muda mrefu zaidi ikilinganishwa na maneno mengine. Hyman (1975) anabainisha kuwa kuna aina mbili za mkazo: mkazo katika neno na mkazo katika sentensi. Katika lugha kama Kiingereza, mkazo unaweza kuwekwa popote katika neno (mkazo huru), wakati Kiswahili kinatumia mkazo fungwa, ambapo mkazo huwekwa kwenye silabi ya pili kutoka mwisho wa neno. Hivyo, mkazo huu unaathiri uelewa na matumizi ya lugha husika, na ni muhimu kwa wanafunzi wa Kiswahili kuelewa taratibu hizi ili kuboresha ujuzi wao wa lugha. Hii ina maana kwamba kuelewa mkazo ni muhimu kwa wanafunzi wa Kiswahili, hasa wale wanaotoka katika lugha zenye mkazo huru, kwani wanaweza kukutana na changamoto katika utamkaji wa maneno (Bachman, 1990). Hivyo, inahitajika kujifunza kwa makini mkazo wa Kiswahili ili kufanikiwa katika mawasiliano.

Kwa upande wa Kinyarwanda, mkazo unatumika tofauti kidogo. Lugha hii ina utaratibu wa mkazo ambao unaweza kuwa na shadda, inayoweza kubadilisha maana ya maneno. Katika Kinyarwanda, mkazo unaweza kuathiri uelewa wa maneno na mawasiliano kwa ujumla. Kwa mfano, shadda inatumika kuongeza nguvu ya silabi fulani, hivyo kuleta tofauti ya maana kati ya maneno yanayotamkwa. Hii inamaanisha kwamba wanafunzi wa Kiswahili wanaotoka kwenye mazingira ya Kinyarwanda wanahitaji kuelewa tofauti hizi ili kufanikiwa katika ujifunzaji wa Kiswahili.

Tofauti ya mkazo kati ya Kiswahili na Kinyarwanda inaweza kuleta athari kubwa katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa Kinyarwanda. Kwa kuwa Kiswahili hutumia mkazo fungwa, ambapo mkazo huwekwa kwenye silabi ya pili kutoka mwisho wa neno. Kinyarwanda kinaweza kutumia shadda ambayo huongeza nguvu ya silabi na kubadilisha maana ya maneno, tofauti hizi za kifonolojia zinaweza kusababisha matatizo ya utamkaji na uelewa wa lugha. Kwa mfano, mwanafunzi wa Kinyarwanda anaweza kupata ugumu katika kutambua au kuiga mkazo

wa Kiswahili kwa usahihi. Ni kwa sababu hii, kama inavyobainishwa na Tumbo-Masabo (1999), tuliamua kufanya utafiti kuhusu athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili, ili kuimarisha ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

### 2.3.3 Lafudhi

Lafudhi ni kipengele muhimu katika fonolojia ya lugha, ikihusiana na namna ya kutamkwa na kusikika kwa sauti na jinsi inavyoathiri utambulisho wa msemaji. Lafudhi inabeba maana ya kijamii na kijiografia, ikionesha jinsi mazingira ya mtu yanavyoweza kuathiri matamshi yake. Katika muktadha huu, lafudhi inaweza kutambuliwa kama alama ya utambulisho wa kisarufi, ambapo msemaji anajitambulisha kupitia mtindo wa sauti anautumia, unaotokana na muktadha wa kijamii na kijiografia anamoishi (Khamis, 2015; Tumaneng, 2019).

Katika Kiswahili, lafudhi ina umuhimu mkubwa katika kubainisha tamaduni na mitindo tofauti ya lugha. Kwa mfano, kuna lafudhi mbalimbali zinazoweza kuonekana kati ya wasemaji wa Kiswahili kutoka maeneo tofauti kama vile Pwani, Kaskazini, na Kusini mwa Tanzania. Kila lafudhi ina sifa zake za kipekee zinazoweza kutambulika kwa urahisi na wasikilizaji, hivyo kuonesha tofauti za utamaduni na mawasiliano. Hii inadhihirisha jinsi lafudhi inavyoweza kuwa kiashiria cha utambulisho na kutambua muktadha wa msemaji (Mugambi, 2018).

Katika Kinyarwanda, lafudhi pia ina umuhimu katika utamaduni na mawasiliano. Watu kutoka sehemu mbalimbali za Rwanda wana lafudhi tofauti, ambapo lafudhi ya mahali fulani inaweza kutofautiana na ile ya pengine nchini Rwanda. Kila lafudhi inatoa picha ya asili ya msemaji na mazingira yake ya kijiografia, hivyo inachangia katika utambulisho wa kijamii. Lafudhi ya Kinyarwanda inajulikana kwa matumizi ya sauti na kuzingatia vivutio vya sauti, ambavyo vinaweza kubadilisha maana ya maneno (Twagiramungu, 2020).

Tofauti kati ya lafudhi katika Kiswahili na Kinyarwanda inaakisi muktadha wa lugha na utamaduni wa wasemaji. Katika Kiswahili, lafudhi inategemea sana eneo na utamaduni wa mzungumzaji, huku ikiwa na mabadiliko makubwa kati ya jamii za wasemaji (Twagiramungu, 2020). Kwa upande mwingine, Kinyarwanda lina lafudhi ambazo zinaweza kuonesha tofauti za kijiografia na kijamii, lakini pia zinahusiana na matumizi ya sauti za pekee, kama vile shadda,

ambazo si za kawaida katika Kiswahili. Kwa hivyo, kutokana na maandiko tuliyopitia, tuliamua kufanya utafiti wetu ili tuchunguze athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili.

### 2.3.4 Toni

Matumizi ya toni katika lugha ni kipengele muhimu kinachohusiana na kidatu darajia ya neno, ambapo toni inaweza kuwa ya kifonetiki au kileksia. Toni ya kifonetiki inazingatia matamshi sahihi ya neno, wakati toni ya kileksia inahusisha maana za kimsingi za neno. Lugha nyingi za Kibantu, kama Kikuyu, zinaonesha wazi tofauti kati ya toni sahili na toni mseto. Toni sahili inahusiana na silabi, ambapo kila silabi ina toni yake. Kwa mfano, neno "mwaki" katika Kikuyu lina toni mbili zinazolingana na silabi zake mbili, na ruwaza ya toni itategemea maana ya neno (Halliday, 1970). Toni mseto, kwa upande mwingine, hujumuisha viwango viwili au zaidi vya toni ndani ya silabi moja, kama vile neno "hia" linaloonesha upinde wa toni katika lugha hiyo (Hyman, 1975). Matumizi ya toni yanaonesha maingiliano kati ya mofolojia na semantiki, ambapo toni zinapokuwa na maana tofauti, hubainisha pia sifa za kimofolojia kama viambishi awali na misingi ya maneno.

Katika lugha ya Kiswahili, toni si muhimu sana katika kuashiria maana kama ilivyo katika lugha zingine za Kibantu. Badala yake, Kiswahili kinazingatia mpangilio wa maneno na muundo wa sentensi katika kutoa maana. Hata hivyo, toni inaweza kutumika kuonesha hisia au kusisitiza jambo fulani. Kwa mfano, kauli kama "ndiyo" inaweza kutamkwa kwa toni tofauti kulingana na mtazamo wa msemaji. Toni ya juu inaweza kuonesha uthibitisho, wakati toni ya chini inaweza kuonesha udhabiti au kutokuwa na uhakika (Khamis, 2015). Hivyo, toni hutumika zaidi katika mazingira ya pragmatiki na siyo kwa kiwango kikubwa katika kubainisha maana za kimsingi za neno kama ilivyo katika lugha nyingine zenye toni kama Kinyarwanda au Kikuyu.

Kwa upande wa Kinyarwanda, toni ni kipengele muhimu sana kwa lugha hii, ambapo toni tofauti zinaweza kubadilisha kabisa maana ya neno. Kinyarwanda kina mfumo wa toni nyingi, ambapo neno moja linaweza kuwa na maana tofauti kulingana na toni inayotumika. Kwa mfano, neno "umwami" linaweza kumaanisha "mfalme" au maana nyingine kabisa kulingana na toni (Twagiramungu, 2020). Hii inaonesha kwamba katika Kinyarwanda, toni ni sehemu muhimu ya mfumo wa sarufi na semantiki. Wanafunzi wanaojifunza lugha yenye toni kama Kinyarwanda

lazima waelewe vizuri matumizi ya toni ili kufikisha maana halisi ya maneno na sentensi wanazotamka. Hali hii inafanya toni kuwa kipengele muhimu katika lugha ya mawasiliano ya kila siku.

Tofauti kubwa kati ya Kiswahili na Kinyarwanda inajitokeza katika jinsi toni zinavyotumika kubainisha maana. Wakati Kiswahili kinategemea zaidi mpangilio wa maneno na mofolojia ili kutoa maana, Kinyarwanda kinategemea sana toni kama kipengele cha kimsingi cha lugha. Katika Kinyarwanda, matumizi mabaya ya toni yanaweza kubadilisha kabisa maana ya neno, hali ambayo si kawaida katika Kiswahili. Kwa hiyo, katika utafiti wetu, tumeamua kuchunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili. Kwa kutumia utafiti huu, tunalenga kuona jinsi wanafunzi wanaotumia Kinyarwanda kama lugha ya kwanza wanavyoathiriwa na toni za lugha hiyo katika kujifunza na kutumia Kiswahili sanifu.

### 2.3.5 Mfuatano wa Sauti Kuunda Silabi

Mfuatano wa sauti kuunda silabi ni mpangilio wa sauti za lugha ambao huruhusu kutamkwa kwa silabi kwa njia inayokubalika katika lugha husika. Silabi kawaida huundwa na kiini (ambacho ni irabu) na konsonanti inayoweza kutangulia au kufuata irabu hiyo. Hata hivyo, lugha tofauti zina kanuni tofauti za kifonolojia kuhusu jinsi sauti hizi zinavyoweza kufuatana. Kwa mujibu wa Massamba (1996), lugha nyingi zinafuata taratibu maalum ambazo husaidia katika kuhakikisha uundaji wa silabi unafuata kanuni za lugha hiyo, na mfuatano huu unaweza kuathiri usahihi wa matamshi.

Katika Kiswahili, mfuatano wa sauti kuunda silabi unaruhusu kufuatana kwa irabu mbili katika silabi moja, kama vile kwenye neno "saa" au "ua," ambapo irabu mbili zinaweza kufuatana bila shida. Aidha, Kiswahili pia huruhusu kufuatana kwa konsonanti mbili katika silabi moja, kama vile kwenye maneno kama "bwana" au "mchezo" ambapo konsonanti kama /b/ na /w/ au /m/ na /ch/ zinaweza kufuatana. Hii ni tofauti na baadhi ya lugha nyingine, ambapo mfuatano wa sauti hizo ungekuwa mgumu kutamkwa au kutoeleweka (Massamba, 1996).

Kwa upande wa lugha ya Kinyarwanda, mfuatano wa sauti kuunda silabi una vizuizi zaidi. Katika Kinyarwanda, irabu mbili haziwezi kufuatana isipokuwa katika baadhi ya maneno machache kama vile "saa" au kwenye vihisishi. Aidha, irabu mbili zisizofanana, kama vile /a/ na

/e/, haziwezi kufuatana katika silabi moja. Pia, Kinyarwanda ina vizuizi vya kipekee kwa konsonanti; kwa mfano, sauti ya /m/ haiwezi kufuatwa na konsonanti kama vile /s/, /z/, /n/, /t/, /d/, /r/, au /l/ (Kimenyi, 2002). Hii ni tofauti kubwa ikilinganishwa na Kiswahili, ambapo mfuatano wa /m/ na konsonanti hizi ni wa kawaida kabisa, kama inavyoonekana kwenye maneno kama "mtoto" au "mzigo."

Tofauti kati ya mfuatano wa sauti kuunda silabi katika Kiswahili na Kinyarwanda ni dhahiri. Wakati Kiswahili huruhusu kufuatana kwa irabu mbili na pia mchanganyiko wa konsonanti mbalimbali kama vile /m/ ikifuatiwa na konsonanti nyingine, Kinyarwanda lina vizuizi vikubwa zaidi katika mchanganyiko huu wa sauti. Kwa mfano, Kinyarwanda hairuhusu kufuatana kwa irabu mbili zisizofanana au sauti ya /m/ ikifuatiwa na konsonanti fulani, ilhali Kiswahili huruhusu miunganiko hii kwa uhuru zaidi. Tofauti hizi za kifonolojia zinadhihirisha utofauti wa kimatamshi baina ya lugha hizi mbili, na ni msingi wa utafiti wetu kuhusu uchunguzaji athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera nchini Rwanda.

**2.3.6 Otografia ya Kiswahili na Kinyarwanda**

Otografia ni mfumo wa mwandiko unaoendana na kanuni za kila lugha, ikiwemo jinsi sauti zinavyowakilishwa kwa maandishi. Katika Kiswahili, otografia yake hutumia alfabeti ambazo zinatumika kuwakilisha sauti mbalimbali za lugha hiyo. Kwa kawaida, kuna uwiano wa moja kwa moja kati ya jinsi neno linavyotamkwa na linavyoandikwa, hali inayoifanya otografia ya Kiswahili kuwa rahisi zaidi kueleweka. Hii inamaanisha kuwa matamshi ya neno mara nyingi yanafanana na maandishi, jambo linalorahisisha kujifunza na kufundisha lugha hii (Massamba, 1996). Kwa upande mwingine, otografia ya Kinyarwanda nayo hutumia alfabeti ya Kilatini lakini inakabiliana na changamoto za kipekee, ikiwemo kuonesha tofauti za sauti zenye toni, ambazo zinaweza kubadilisha maana ya neno, jambo ambalo halipo kwenye Kiswahili.

Fonolojia ya Kiswahili ni rahisi ikilinganishwa na Kinyarwanda. Lugha ya Kiswahili ina irabu tano kuu: /a/, /e/, /i/, /o/, na /u/, ambazo hutumika kwa mpangilio rahisi katika maneno. Katika lugha hii, hakuna mfuatano mgumu wa sauti za konsonanti au irabu, na hivyo kufanya maneno kuwa na silabi rahisi kusomwa na kuandikwa. Kwa upande wa Kinyarwanda, kuna vizuizi vya mfuatano wa sauti, hasa irabu na konsonanti, ambavyo haviruhusiwi kufuatana katika maneno

fulani. Pia, Kinyarwanda kina mfumo wa toni, ambapo toni tofauti zinaweza kubadilisha maana ya neno, jambo linalofanya otografia yake kuwa ngumu zaidi kwa watumiaji wapya (Kimenyi, 2002).

Ingawa Kiswahili na Kinyarwanda zote ni lugha za Kibantu, kuna mfanano na tofauti kadhaa kati ya mifumo yao ya mwandiko na fonolojia. Lugha zote mbili zinatumia alfabeti ya Kilatini na zina irabu tano sawa, lakini Kiswahili ni lugha yenye uwiano bora kati ya matamshi na mwandiko. Hali hii inafanya kuwa na otografia inayofuata kanuni rahisi na isiyo na vizuizi vingi vya mfuatano wa sauti. Kwa upande mwingine, Kinyarwanda kina mfuatano mgumu wa irabu na konsonanti, na pia kinahitaji toni maalum za kifonolojia kuonesha maana halisi ya neno. Hii inafanya otografia ya Kinyarwanda kuwa changamano zaidi na inahitaji uelewa mzuri wa kanuni za lugha hiyo ili kuandika na kutamka kwa usahihi (Kimenyi, 2002).

Dhima ya irabu katika Kiswahili na Kinyarwanda inaonesha utofauti mkubwa. Katika Kiswahili, irabu hutumika kwa urahisi, ambapo zinaweza kufuatana bila matatizo, kama inavyoonekana kwenye maneno kama "saa" au "ua." Hata hivyo, Kinyarwanda kina vizuizi vya kufuatana kwa irabu ambapo irabu mbili haziwezi kufuatana kirahisi isipokuwa ziwe sawa au zitenganishwe na konsonanti. Hii inadhihirisha kuwa, ingawa lugha zote mbili zina irabu sawa, jinsi zinavyotumika ni tofauti.

Katika Kinyarwanda, irabu pia huchukua jukumu muhimu katika kuonesha toni, ambayo inaweza kubadilisha kabisa maana ya neno kulingana na toni inayotumika (Kimenyi, 2002). Hivyo, otografia ya lugha hizi mbili, ingawa inatumia herufi zinazofanana, ina kanuni tofauti zinazotokana na mifumo yao ya fonolojia. Hii inaweza kuleta athari katika ujifunzaji wa Kiswahili ambapo wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kinyarwanda wanaweza kuathiriwa na lugha yao ya kwanza kiasi kwamba wanaweza kutumia otografia ya Kiswahili kama wanavyotumia ya Kinyarwanda. Wazo hili lilitupa shauku ya kutaka kufanya utafiti ili tuchunguze ikia kuna athazi za kiotografia za Kinyarwanda ambazo huathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Bugesera nchini Rwanda.

## 2.4 Athari za Kifonolojia za Lugha za Kibantu katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili

Lugha ya kwanza ni lugha ambayo mtu hujifunza awali kabisa tangu utotoni mwake au akiwa mdogo . Pia inajulikana kama lugha ya mama au lugha ya asili. (Derakhshan & Karimi, 2015). Lugha ya kwanza ni lugha ambayo mtu anaweza kuwa na uwezo wa kuwasiliana nayo kwa ufasaha zaidi kuliko lugha nyingine yoyote. Mara nyingi, lugha ya kwanza inahusishwa na utambulisho wa kitamaduni na kijamii wa mtu. Hivyo, kwenye tasnifu hii, lugha ya kwanza imeelezwa kama lugha ambayo mtu huipata kabla ya lugha yoyote ile.

Athari ya kifonolojia ya lugha za Kibantu kama vile Kiolusuba, Kijita na Kisamia kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili inajumuisha uchopekaji, ambapo kipashio kinaongezwa kwenye neno (Wanjala, Mukoyani & Agaba, 2023). Wanafunzi wanaotumia lugha za Kibantu kama lugha zao za kwanza wanaweza kukumbana na changamoto ya kuingiza sauti za ziada katika maneno wanaposema au kuandika Kiswahili (Wanjala na wenzake, whj). Watafiti hawa wanabainisha kuwa katika uchambuzi, wanafunzi kama hawa mara nyingi wanakabiliwa na uchopekaji hasa kwa sauti za /n/ na /m/. Hata hivyo, kuna pia maneno ambayo yanadhihirisha uchopekaji wa irabu hususani sauti ya /u/ (Wanjala, Mukoyani& Agaba, whj). Hali hii inaweza kuwa changamoto kwa wanafunzi hawa katika kujenga ufasaha wa lugha ya Kiswahili, kwani inaweza kusababisha utamkaji usio sahihi na uelewa mdogo wa muundo wa maneno.

Wanjala na wenzake (whj) wanachunguza athari za kifonolojia zinazotokana na lugha za Kibantu kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili kwa jumla, bila kuzingatia lugha za Kibantu mahususi. Maelezo yao yanaonesha kuwa kuongeza fonimu kwenye maneno ni moja ya athari za lugha za Kibantu ambazo zinaweza kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili.

Kwa hivyo, utafiti wetu ulilenga kubaini kama athari hii ni sehemu ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda zinazochangia kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari katika wilaya ya Bugesera,nchini  Rwanda.

Athari ya kifonolojia ya pili inayotokana na lugha za Kibantu kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili ni udondoshaji. Huu ni mchakato wa kuondoa kipashio kutoka kwenye neno. Udondoshaji hutokea wakati kipashio kiondolewa kwa namna inayoenda kinyume na taratibu za lugha husika (Ontieri, 2010). Tofauti katika utaratibu wa mfuatano wa sauti kati ya lugha ya kwanza na Kiswahili inaweza kusababisha kuondolewa kwa sauti au silabi nzima, hivyo kuleta

kasoro katika maneno. Sauti zinazokumbwa na udondoshaji mara nyingi ni sauti za nazali, hasa pale zinapokuwa kwenye muktadha wa sauti mwambatano. Mukuthuria (2004) na Ngugi (2007) wanasema kwamba sauti mwambatano hutoa changamoto na hivyo huweza kusababisha makosa katika muundo wa maneno yanayojumuisha sauti hizi.

Kulingana na maelezo haya, , kuondoa sauti fulani katika maneno ya Kiswahili ni athari ambayo hutokana na lugha za kwanza za wanafunzi wa Kiswahili wenye asili ya lugha za Kibantu. Athari hii inaweza kuwa changamoto kwa wanafunzi wanaotumia lugha za Kibantu wanapojifunza Kiswahili, kwani inaweza kusababisha utamkaji usio sahihi na uelewa mdogo wa muundo wa maneno. Kwa hiyo, tulipata shauku ya kufanya utafiti wetu ili kuchunguza ikiwa udondoshaji ni mojawapo ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilikwa wajifunzaji wa shule za sekondari wilayani Bugesera.

Athari ya tatu ya kifonolojia ya lugha za Kibantu kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili inajumuisha ubadilishaji wa fonimu. Kwa mujibu wa Wanjala na wenzake (2023), ubadilishaji wa fonimu ni mchakato ambapo fonimu moja inabadilishwa na nyingine katika matumizi ya lugha. Kwa wanafunzi wa Kiswahili kutoka jamii za Kibantu, kuna makosa yanayotokea ambayo yanahusiana na ubadilishaji wa fonimu, kama vile kubadilishana nafasi kati ya fonimu za /r/ na /l/. Kwa mfano, badala ya kutumia fonimu sahihi ya /r/, wanafunzi wanaweza kutumia /l/ katika maneno kama "rafiki" badala ya "lafiki" au kutumia /r/ badala ya /l/ katika maneno kama "lundo" badala ya "rundo" (Ontieri, khj).

Maelezo haya yanaonesha kwamba fonolijia ya lugha za Kibantu huathiri ujifunzaji wa Kiswahili pale ambapo wanafunzi hudilisha fonimu kwa fonimu nyingine kimakosa. Hali kama hii inaweza kusababisha kuchanganyikiwa katika utamkaji wa maneno na kuvuruga uelewa wa wasikilizaji, hivyo kuharibu mawasiliano sahihi.

Kwa hiyo, kutokana na kwamba Wanjala na wenzake (whj) pamoja na Ontieri (khj) wamejadili athari za kifonolojia kutoka lugha za Kibantu ambazo si Kinyarwanda, utafiti huu utaongeza maarifa kwa kuchunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari katika wilaya ya Bugesera.

Mwisho, wanafunzi wa lugha ya Kiswahili wenye asili ya lugha za Kibantu, wanaathiriwa na mpangilio mbaya wa mofu katika maneno. Ni dhahiri kwamba wanafunzi wa Kiswahili wenye asili ya lugha za Kibantu, kama ilivyooneshwa na Ntawiyanga (2015), wanakumbwa na changamoto ya mpangilio mbaya wa mofu katika maneno.

Hali hii inaathiri uwezo wao wa kuzungumza na kuandika Kiswahili ipasavyo. Wanafunzi hawa, hasa nchini Rwanda, mara nyingi hujikuta wakiathiriwa na athari hii ambapo huweka mofu katika nafasi ambazo si sahihi kulingana na muundo wa lugha. Sababu kuu ya hali hii ni kutaka kuunda maneno kwa kufuata muundo wa lugha yao ya asili, Kinyarwanda. Kwa mfano, badala ya kusema "nilipoona", wanaweza kusema "nilionapo" (Ntawinyanga, khj). Pengine, badala ya kusema "aliyekuja", wanaweza kusema "alikujaye".

Maelezo haya yanaonesha kwamba wanafunzi wa Kiswahili nchini ya Rwanda huathiriwa na Kinyarwanda pale ambapo wanataka kuzipanga mofu za Kiswahili kwenye maneno kama wanavyozipanga zile mofu za Kinyarwanda. Upangaji na mofu wa aina hii mara nyingi huweza kuvuruga maana ya maneno na hivyo kuzuia ujumbe wanaotaka kutoa kueleweka vyema. Kutokana na hali hii, tuliamua kufanya utafiti wetu uli tuchunguze ikiwa upangaji usio sahihi wa foni katika maneno ni mojawapo ya athari za kofonolojia za Kinyarwanda zinazowaathiri wanafunzi wanapojifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule katika wilaya ya Bugesera.

Maelezo yaliyotolewa yanaelezea kwa undani athari za kifonolojia za lugha za Kibantu katika mchakato wa kujifunza Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Athari hizo ni pamoja na uchopekaji, udondoshaji na mpangilio mbaya wa fonimu katika maneno. Hata hivyo, tafiti zilizofanyika hazijajumuisha uchambuzi wa kina wa mikakati maalum ya ufundishaji au hatua za kuingilia kati ili kushughulikia athari hizi za kifonolojia, hivyo kuacha pengo kubwa katika suluhisho za vitendo kwa walimu. Hivyo basi, utafiti uliofanyika ulikusudia kujaza pengo hili.

### 2.5 Mikakati ya Kuondoa Athari za Kifonolojia za Kibantu katika Ujifunzaji wa Kiswahili

Moja kati ya mikakati muhimu katika kufundisha Kiswahil ni kutoa mazoezi ya kutosha yanayohusiana na fonolojia yake . Mazoezi haya huwapa wanafunzi fursa ya kujifunza sauti, muundo na vipashio vya maneno katika Kiswahili (Kanake & Kobia, 2023). Wanafunzi hupata uelewa wa lugha hiyo na kujenga ufasaha bila kuingiliwa na athari za lugha yao ya asili.

Mazoezi haya pia hutoa mazingira salama kwa wanafunzi kufanya makosa na kujifunza kutokana nayo, huku wakipata uzoefu wa moja kwa moja na muundo wa maneno ya Kiswahili. Hii ni njia muhimu inayoweza kusaidia kuimarisha ujuzi wa lugha miongoni mwa wanafunzi wa asili ya lugha za Kibantu, na hivyo kusaidia kuondoa athari za kifonolojia katika ujifunzaji wa Kiswahili.

Maelezo haya ni ithibati kuwa utumiaji wa mazoezi mengi kuhusu fonolojia ya Kiswahili ni mojawapo ya mikakati ya kuepukana na athari za lugha za Kibantu katika Ujifunzaji wa Kiswahili. Ila, hapa mtu anaweza kujiuliza ikiwa mkakati huu unaweza kutumiwa kwa wanafunzi wa Kiswahili wenye asili ya lugha ya Kibantu yoyote ile.

Utafiti wetu ulikusudia kuchunguza namna ambavyo mazoezi ya kutosha kuhusu fonolojia ya Kiswahili yanaweza kutumiwa ili kuepukana ana athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Bugesera.

Mkakati wa pili ni kufundisha tofauti kati ya fonolojia ya Kiswahili na ya lugha ya Kibantu. Huu ni mkakati muhimu kwa wanafunzi wa asili ya lugha za Kibantu wanapojifunza Kiswahili (Mukuthuria, 2004). Hii ni kwa sababu ufahamu mzuri wa tofauti hizi unaweza kusaidia katika kuvunja vizuizi vya kifonolojia na kuboresha ufasaha wao wa Kiswahili. Wanafunzi wanaojua jinsi sauti, muundo na vipashio vya maneno vinavyotofautiana kati ya lugha hizo wanaweza kuepuka makosa ya kifonolojia na kuboresha mawasiliano yao kwa lugha mpya.

Kutokana na hoja ya hapo juu, ni lazima wanafunzi wafundishwe tofauti iliyopo kati fonolojia ya lugha yao ya kwanza na lugha ya Kiswahili. Jambo hili linaweza kuwa msingi muhimu katika kujenga ustadi mzuri wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa asili ya lugha za Kibantu.

Licha ya maelezo haya, bado, Mukuthuria (khj) hajabainisha waziwazi taratibu za kutekeleza mkakati huu hahasa kwa wanafunzi wanaojifunza lugha nyingine za Kibantu kama vile Kinyarwanda. Hivyo basi, tulipata shauku ya kufanya utafiti ili kuchunguza ikiwa ufundishaji wa tofauti kati ya fonolojia ya Kinyarwanda na ya Kiswahili ni mojawapo ya mikakati ya kuondoa athari za kifonolojia za kinyarawanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari katika wilaya ya Bugesera, nchini Rwanda.

Mkakati wa tatu muhimu katika kuondoa athari za kifonolojia za lugha ya Kibantu kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili ni kuanzisha klabu za Kiswahili katika shule. Kwa mujibu wa Niyomugabo (2016), kupitia klabu hizi, wanafunzi wanapewa fursa ya kujadiliana na kuzungumza Kiswahili kwa mazungumzo ya kila siku. Hii inawasaidia kujenga ujasiri katika matumizi ya Kiswahili na kuwawezesha kuzoea lugha hiyo bila kuingiliwa na mitindo ya kifonolojia ya lugha zao za awali. Klabu za Kiswahili pia zinatoa mazingira mazuri ya kujifunza ambapo wanafunzi wanaweza kushirikiana na kusaidiana, hivyo kukuza ujuzi wao wa lugha kwa njia ya vitendo. Kulingana na mkakati huu, ili kuondoa athari za kifonolojia za lugha za kibantu katika ujifunzaji wa Kiswahili, ni lazima wanafunzi wajengewe mazingira mabayo yatawawezesha kupata fursa ya kutosha ya kuzungumza Kiswahili. Hata kama maelezo haya yametolewa, Niyomugabo (khj) haoneshi namna ambavyo mkakati huu unaweza kutumiwa na walimu wakiwemo walimu wa shule kwenye nchi ya Rwanda ambapo ufupi wa muda huwezi kuwaruhusu walimu kuhudhuria shughuli za klabu za Kiswahili. Kutokana na pengo hili, tuliamua kufanya utafiti ili tuchunguze ikiwa uanzishaji wa klabu unaweza kushiriki katika kuondoa athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili kwenye nchi ya Rwanda.

Pia, tulikusudia kutoa mwongozo wa utumiaji wa uundaji wa klabu katika kuondoa athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

Mkakati wa nne wenye ufanisi wa kupunguza athari za kifonolojia kutoka lugha za Kibantu katika ujifunzaji wa Kiswahili ni kutumia TEHAMA. Kutokana na mabadiliko ya kidijitali, TEHAMA inaweza kuwa zana yenye manufaa katika kuwasaidia wanafunzi kujifunza Kiswahili kwa njia inayoshawishi na inayokubaliana na mazingira yao ya kiteknolojia (Msigwa & Vicent, 2021).

Programu za TEHAMA na majukwaa ya mtandaoni yanaweza kutumika kuunda mazingira ya kujifunzia yanayovutia ambapo wanafunzi wanaweza kupata mazoezi ya kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika Kiswahili. Vilevile, TEHAMA inaweza kutumiwa kutoa zana za kujifunzia kama vile programu za utamkaji, mazoezi ya kuangalia matamshi na michezo ya

kujifunza lugha ambayo inawasaidia wanafunzi kuzoea na kufanya mazoezi ya sauti za Kiswahili (Msigwa & Vicent, whj).

Kwa msingi wa maelezo yaliyotolewa, TEHAMA inaweza kuwa njia rahisi na bora ya kusaidia wanafunzi kuboresha ustadi wao wa Kiswahili na kupunguza athari za kifonolojia kutoka lugha zao za asili. Hata hivyo, licha ya maelezo haya, hakuna mwongozo ulioainishwa ambao walimu wanaweza kutumia ili kuepuka athari za lugha za Kibantu wakati wanapofundisha Kiswahili kwa wanafunzi kutoka katika asili za lugha za Kibantu.

Kwa hiyo, hali hii, tulipata shauku ya kufanya kuchunguza ikiwa utumiaji wa TEAHAMA unafaa katika kuondoa athari za kifonolojia za lugha za Kibantu katika ufundishaji wa Kiswahili. Utafiti pia ulikusudia kutoa utaratibu wa utumiaji wa TEHAMA katika kuondoa athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa shule za upili katika wilaya ya Bugesera kwenye nchi ya Rwanda.

### 2.7 Mapengo ya Utafiti

Kama ilivyodhihirishwa, kwenye tafiti zilizofanywa na watafiti wa awali kulidhihirika mapengo tofauti ambayo yatajazwa na utafiti huu. Kwanza, tafiti za Kimenyi (2003) & Mohochi (2011) zinabainisha kuwa ufundishaji wa Kiswahili Kwenye nchi ya Rwanda unaathiriwa na changamoto kadhaa bila kuonesha mikakati ya kuondoa changamoto hizo. Tatu, Mukuthuria (2004), Ngugi (2007), Derakhshan & Karimi (2015) & Wanjala, na wenzake (2023) wanazungumzia athari za kifonolojia za lugha za Kibantu katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Lugha ambazo wanazizungumzia ni tofauti sana na lugha ya Kinyarwanda. Isitoshe, tafiti za Kimenyi (2003), Ntawiyanga (2015), Niyomugabo (2016) na Mukashyaka (2023) zinajadili athari za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilikwa ujumla bila kutoa msisitizo wa kutosha kwenye athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika mchakato wa kujifunza Kiswahili.

Hatimaye, Kanake na Kobia (2023), Mukuthuria (2004), Niyomugabo (2016), na Msigwa na Vincent (2021) wanataja mikakati ya kupunguza athari za kifonolojia za lugha za Kibantu katika mchakato wa kujifunza Kiswahili bila kuzingatia lugha ya Kinyarwanda. Aidha, watafiti hawa hawatoi taratibu maalum ambazo walimu wa Kiswahili wanaweza kufuata katika kutekeleza

mikakati hii. Hivyo basi, utafiti wetu ulikusudia kuchunguza kwa kina athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari katika wilaya ya Bugesera kwenye nchi ya Rwanda.

**2.8 Kiunzi cha Nadharia**

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi, ambayo inalinganisha na kutofautisha lugha mbili ili kuelewa jinsi zinavyoshabihiana na kutofautiana (Lado, 1957). Nadharia hii inazingatia athari za lugha ya kwanza (L1) kwenye mwanafunzi wa lugha ya pili (L2) katika maeneo kama kimsamiati, kisarufi, kimatamshi, na kisemantiki. Athari hizi za lugha ya kwanza zinaweza kuwa na athari chanya au mbaya kwenye mchakato wa kujifunza lugha ya pili (Lado, khj).

Kulingana na Lado (khj), Uchanganuzi Linganuzi hutekelezwa kwa kufuata hatua zifuatazo. Kwanza, kutoa maelezo yanayofaa kuhusu muundo wa lugha mbili zinazochanganuliwa. Halafu, kuteua vipengele vya lugha hizo ambavyo vitafanyiwa ulinganifu. Hatimaye, kufananisha na kutofautisha vipengele hivyo katika lugha hizo mbili. Kama inavyoelezwa na Kanake & Kobia (2023), Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi inakuwa na mihimili miwili.

Mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi, ambao unaangazia athari za lugha ya kwanza (L1) kwenye kujifunza lugha ya pili (L2), ulitumika katika utafiti huu kwa kuchunguza makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Bugesera wanapojifunza Kiswahili. Katika hatua hii, ulinganifu kati ya fonolojia ya Kinyarwanda na Kiswahili ulifanyika kwa kuchambua mifano ya matamshi ya wanafunzi, na kutambua makosa yanayosababishwa na athari za lugha ya kwanza. Kwa mfano, wanafunzi wengi walikuwa na matatizo ya kutamka irabu za Kiswahili kama zilivyo kwa sababu fonolojia ya Kinyarwanda ina toni tofauti za irabu. Matokeo haya yalisaidia walimu kubuni mbinu bora za kufundisha matamshi sahihi ya Kiswahili kwa kujiepusha na makosa haya.

Pia, mhimili huu ulitumika kutabiri ni makosa gani yanaweza kujitokeza katika vipengele vingine vya lugha kama vile msamiati na sarufi. Kwa mfano, lugha ya Kinyarwanda inatumia majina ya vitu kwa jinsi tofauti na Kiswahili, na hivyo wanafunzi walionekana kuwa na ugumu wa kutofautisha jinsia ya maneno katika Kiswahili, hali ambayo ilisababisha makosa ya

matumizi ya maneno ya jinsia. Hivyo, kulinganisha mifumo ya lugha hizi mbili kulirahisisha mchakato wa kutabiri na kubuni mikakati ya kuepuka makosa hayo.

Mhimili wa pili wa nadharia hii, unaosisitiza kufundisha wanafunzi ulinganifu kati ya lugha ya kwanza na ya pili, ulitumika kwa kuwasaidia wanafunzi kuelewa vipengele vya lugha ambavyo vinafanana kati ya Kinyarwanda na Kiswahili. Kwa mfano, walimu waliwaonesha wanafunzi kuwa irabu tano kuu katika Kiswahili ni sawa na zile za Kinyarwanda, hivyo wanafunzi walipata urahisi katika kujifunza matamshi sahihi ya irabu hizo katika Kiswahili. Uelewa huu wa maeneo yanayofanana uliwawezesha wanafunzi kuboresha matamshi yao na hivyo kupunguza makosa yaliyotokana na utofauti wa kifonolojia.

Kwa kuongezea, ulinganifu huo ulitumika kuonesha tofauti katika vipengele ambavyo havifanani, kama vile mifumo ya toni. Katika Kinyarwanda, toni zinatumika kubadilisha maana ya maneno, lakini Kiswahili hakina toni hizo, jambo lililohitaji wanafunzi kuelekezwa wazi kwamba maneno ya Kiswahili hayaathiriwi na toni. Kwa hivyo, walimu walitumia ulinganifu huu kuwasaidia wanafunzi kuelewa ni maeneo gani yanahitaji makini zaidi katika kujifunza Kiswahili, na walisaidia kuboresha uelewa wa wanafunzi wa mfumo wa kifonolojia wa lugha hii ya pili.

### 2.9 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura ya pili imezungumzia mengi kuhusu mapitio ya maandiko. Sura hii ina sehemu zifuatazo: utangulizi, dhana fonolojia, dhana ya fonimu, vipengele vya fonolojia, athari kifonolojia za lugha za Kibantu katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na mikakati ya kuondoa athari za kifonolojia za Kibantu katika ujifunzaji wa Kiswahili, mapengo ya utafiti, kiunzi cha nadharia, muhtasari wa sura ya pili.

# SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu zilizotumika katika utafiti huu. Vipengele vya sehemu hii ni: utangulizi, paradima ya utafiti, mpangilio wa utafiti, eneo la utafiti, kiwango, sampuli, mbinu za kukusanya data, aina za data, vifaa vya utafiti, uchambuzi wa data, uhalali na uthabiti na muhtasari wa sura ya tatu.

## 3.1 Paradima ya Utafiti

Paradima ya utafiti ni mfumo wa falsafa unaosimamia utafiti, ukionesha imani za mtafiti kuhusu ukweli na utafiti (Abdul & Alharthi, 2016). Paradima inaathiri jinsi mtafiti anavyounda nadharia na kutumia njia za utafiti katika mradi wake. Lengo kuu la utafiti lilikuwa kuchunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Ili kutimiza lengo hili pamoja na malengo mahususi, paradima ya ufasiri ilitumiwa.

Paradima ya ufasiri inasisitiza kwamba watu katika jamii wanaweza kuwa na mitazamo tofauti na uelewa wa mambo, huku ikikataa wazo la ukweli wa pekee na kuamini kwamba kila mtu ana mtazamo wake wa ukweli (Pervin & Mokhtar, 2022). Kwa kuzingatia mtazamo wa paradima ya ufasiri, utafiti huu ulifuatilia athari za fonolojia ya Kinyarwanda katika mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari zilizochaguliwa wilayani Bugesera, Rwanda.

Tulitumia mbinu ya utafiti wa kitaamuli ili kupata uelewa wa kina kuhusu jinsi fonolojia ya Kinyarwanda inavyoathiri uelewa na matumizi ya Kiswahili kwa wanafunzi. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na data za kuaminika, tuliendesha usaili na uchunguzi wa kina na kulinganisha taarifa zitakazokusanywa kutoka kwa washiriki wa taasisi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na walimu na wanafunzi, ili kufikia maelezo yanayokubalika kuhusu suala hili.

Katika utafiti tulioufanya, mtafiti alizingatia pia uwezekano wa washiriki kutoa taarifa ambazo hazieleweki au zinazoweza kuathiriwa na muktadha wao. Hivyo, mbinu ya ushuhudiaji ilitumika kuhakikisha kwamba mtafiti anapata uelewa wa kweli wa jinsi fonolojia ya Kinyarwanda

inavyoathiri mchakato wa kujifunza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari zilizochaguliwa kwenye wilaya ya Bugesera.

Ushuhudiaji ulisaidia kubaini hali halisi ya matumizi ya lugha hizi na kuondoa uwezekano wa upendeleo au taarifa zisizo sahihi zinazoweza kujitokeza. Isitoshe, kwa kuzingatia tofauti za mawazo kati ya watafiti, mtafiti alichambua kwa kina maandishi ya wataalamu mbalimbali na kulinganisha data zilizokusanywa ili kuunda mikakati ya kuondoa athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

Mwisho, utafiti uliwashirikisha walimu na wanafunzi wenye ujuzi, uzoefu na ufahamu wa kina katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Kufanya hivyo kulituwezesha kupata taarifa sahihi na za kina zitakazosaidia kujibu maswali muhimu ya utafiti kuhusu jinsi ya kuboresha mbinu za kufundisha na kujifunza Kiswahili kwa ufanisi zaidi katika muktadha wa fonolojia ya Kinyarwanda.

## 3.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mchakato wa kupanga na kuandaa utafiti kwa ufanisi (Creswell, 2014). Hii ni pamoja na kuchagua maswala ya utafiti, kuweka malengo, kuchagua njia sahihi za kukusanya data, kujenga mpangilio wa maswali ya utafiti na kuandaa muundo wa ripoti ya utafiti.

Usanifu wa utafiti unahakikisha kuwa utafiti una ufanisi, unaoweza kufuatiliwa, na unaoweza kutoa majibu sahihi kwa maswali ya utafiti uliopangwa. Kwa hiyo, kulingana na lengo kuu la utafiti, data za kitaamuli ambazo zilikusanywa, zilichanganuliwa kwa njia ya madondoo yatakayofuatiliwa na maelezo.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Ponera (2019) anasema kwamba eneo la utafiti ni sehemu ya mbinu ya utafiti inayoonesha mwelekeo wa kijiografia na kitaaluma kulingana na mada ya utafiti. Ponera (Khj) anaongeza kwamba eneo la utafiti linapaswa kuashiria mahali ambapo utafiti utatekelezwa. Hivyo, eneo la utafiti katika utafiti huu lilijumuisha shule za sekondari katika wilaya ya Bugesera nchini Rwanda.

Bugesera ni wilaya iliyo karibu na wazungumzaji wengi wa Kiswahili, ambapo ilitarajiwa kwamba athari za Kinyarwanda katika matumizi ya Kiswahili zingekuwa ndogo. Hata hivyo, kutokana na uzoefu wa mtafiti wa kufundisha katika wilaya ya Bugesera, ameona kwamba bado kuna makosa mengi katika matumizi ya Kiswahili. Kwa hivyo, tuliamini kwamba tukibainisha makosa yaliyopo katika matumizi ya Kiswahili katika eneo hili, tutapata fursa ya kusaidia maeneo mengine yaliyo mbali na wazungumzaji wa Kiswahili.

### 3.4 Wango na Sampuli ya Utafiti

Sehemu hii imegawanywa katika kiwango na sampuli ya utafiti. Hivyo, kila sehemu imejadiliwa kwa maelezo hapo chini.

#### 3.4.1 Wango la Utafiti

Wango la utafiti ni kundi la watu, vitu, au matukio ambayo utafiti unalenga kuchunguza (Majid, 2018). Katika utafiti huu, kiwango kilijumuisha walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa shule za sekondari katika Wilaya ya Bugesera, nchini Rwanda.

#### 3.4.2 Sampuli ya Utafiti

Katika utafiti, sampuli hutumiwa kumaanisha wawakilishi kutoka kwenye kundi kubwa la washiriki ili kutoa data inayowakilisha kundi zima (Cresswell, 2014). Sampuli haiwezi kupatikana bila kufanya usampulishaji. Usampulishaji ni hatua ya kuchagua sampuli itakayowakilisha washiriki wote walengwa katika utafiti unaotarajiwa kufanyika (Cresswell, khj).

Kwa hiyo, mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumika. Mbinu hii ni mbinu ya usampulishaji ambayo inahusisha kuchagua sampuli kwa makusudi kutoka kwenye kundi la watu walengwa kulingana na sifa fulani au vigezo vilivyowekwa.

Sampuli ya utafiti ilihusisha wanafunzi wote wa mchepuo wa LFK (Litereture in English, French, Kinyarwanda na Kiswahili) kuanzia kidato cha nne hadi cha sita katika GS Nyiragiseke, Kamabuye, Nyirarukobwa na  Kagasa Mwogo. Shule zilichaguliwa kwa kuwa ndizo zenye wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kutoka kidato cha nne hadi cha sita. Wanafunzi hawa

wanajifunza Kiswahili kama somo la kutahiniwa katika mtihani wa taifa. Hivyo, wanajifunza vipindi sita kila wiki.

Sampuli ya utafiti pia, ilihusisha walimu wa Kiswahili katika shule teule. Idadi ya walimu hao ni saba. Katika uchambuzi na uwasilishaji wa data, tumetumia nambari kutoka moja hadi saba (1-7) ili kutofautisha taarifa walizotoa.

Shule ya sekondari ya Nyiragiseke, na G Kamabuye ni shule ambazo zinakaribiana na mpaka wa Rwanda na Burundi ambapo panafika watumiaji wengi wa Kiswahili. Aidha, shule ya sekondari ya Nyirarukobwa na Kagasa Mwogo ni shule za wilaya ya Bugesera ambazo zinakaribiana na mji wa Kigali ambapo kuna idadi kubwa ya watu wanaozungumza Kiswahili. Kwa hiyo, shule hizi nne ni shule ambazo zina wanafunzi ambao wanabahatika kukutana na wazungumzaji wa Kiswahili mara kwa mara. Hivyo basi, wanafunzi na walimu wa shule hizi walisaidia mtafiti kupata taarifa zote zilizoshiriki katika utimizaji wa malengo mahususi ya utafiti.

### 3.5 Mbinu za Kukusanyia Data

Mbinu za ukusanyaji wa data ni njia zinazotumika kupata taarifa zinazohitajika kutoa matokeo ya utafiti (Majid, 2018). Katika utafiti huu, tulitumia mbinu tatu tofauti za ukusanyaji wa data: ushuhudiaji, uchambuzi wa maandishi, na usaili. Mbinu hizi zilifanywa kwa pamoja ili kukusanya taarifa zitakazosaidia kufanikisha malengo ya utafiti.

#### 3.5.1 Uchanganuzi wa Matini

Uchanganuzi wa matini ni mbinu inayohusisha kutafuta data za utafiti kwa kusoma nyaraka mbalimbali zilizohifadhiwa maktabani, mtandaoni, au sehemu nyinginezo (Bowen, 2009). Katika utafiti huu, mbinu hii ilitumika ambapo mtafiti alizisoma na kuchanganua nyaraka mbalimbali kutoka maktabani, mtandaoni, na maeneo mengine. Kupitia uchanganuzi huu, mtafiti alichunguza tafiti za awali zilizofanywa na watafiti waliotangulia kuhusu athari za kifonolojia za lugha za Kibantu katika ujifunzaji wa Kiswahili. Mbinu hii iliruhusu mtafiti kupata uelewa wa kina kuhusu changamoto hizo na jinsi zinavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Aidha, mtafiti alichambua tafiti zilizolenga mikakati ya kuepukana na athari za kifonolojia za lugha za Kibantu katika ujifunzaji wa Kiswahili. Mwisho, mtafiti alichunguza nyaraka za wanafunzi katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera ili kuchunguza athari za kifonolojia

za Kinyarwanda katika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Mbinu hii ilitumika kukusanya data muhimu kwa ajili ya kufanikisha lengo mahususi la kwanza na la pili la utafiti. Ili kukusanya data kuhusu maoni ya walimu juu ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili na mikakati ya kuepukana na athari hizo, mtafiti alitumia pia mbinu ya usaili

### 3.5.2 Usaili

Usaili ni mbinu muhimu ya kukusanya data, hasa pale ambapo mtafiti anahitaji kupata taarifa za kina kutoka kwa washiriki kuhusu uzoefu, maoni, na mitazamo yao juu ya mada inayochunguzwa (De Fina & Perrino, 2011). Katika utafiti huu, usaili ulifanyika kwa kuhoji walimu wa Kiswahili katika mchepuo wa LFK katika shule za sekondari zilizochaguliwa wilayani Bugesera. Lengo kuu lilikuwa ni kupata maoni ya walimu kuhusu athari za kifonolojia za lugha ya Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili, pamoja na mikakati inayotumiwa na walimu ili kukabiliana na athari hizo.

Data zilizokusanywa kupitia usaili zilihusisha aina mbalimbali za athari za kifonolojia ambazo walimu waliziona kwa wanafunzi wao. Aidha, data hizi zilijumuisha maoni ya walimu kuhusu mikakati wanayotumia kufundisha wanafunzi jinsi ya kuepuka makosa ya kifonolojia. Data hizi zilikuwa muhimu kwa kuelewa changamoto zinazokumba walimu na wanafunzi katika mchakato wa ujifunzaji wa Kiswahili na kutoa mapendekezo ya kuboresha mbinu za kufundisha ili kupunguza athari hizo.

Zaidi ya hayo, mbinu hii peke yake, haikuwezesha mtafiti kupata data za moja kwa moja kuhusu hali halisi ya namna ambavyo fonolojia ya Kinyarwanda huathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Hivyo basi, ili kupata data hizi za moja kwa moja, mtafiti alilazimika kutumia pia mbinu ya ushuhudiaji ili kufahamu hali halisi ilivyo.

### 3.5.3 Ushuhudiaji

Ushuhudiaji ni mbinu ya kukusanya na kurekodi data kwa kuchunguza na kufuatilia matukio, tabia au fenomena kwa njia ya kimfumo (Ciesielska, Boström & Öhlander, 2018). Ushuhudiaji hufanyika kwa lengo la kufanya uchunguzi wa kisayansi au kuelewa dunia yetu kwa ujumla.

Hii ni mbinu ya msingi inayotumika katika utafiti, uchunguzi wa kisayansi na maisha ya kila siku ili kupata ufahamu wa dunia inayotuzunguka. Ushuhudiaji ulitumika pale ambapo mtafiti

alishuhudia somo la Kiswahili likifundishwa kwenye mchepuo wa LFK (kuanzia kidato cha nne hadi cha sita) katika shule zilizoteuliwa. Data zilizokusanywa kupitia mbinu hii zilishiriki katika kubainisha hali halisi ya namna ambavyo fonolojia ya Kinyarwanda huathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

### 3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa

Utafiti ulikusanya data za aina mbili ambazo ni data za msingi na upili.

#### 3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi ni aina ya data zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine hapo awali. Mat-Roni, Merga, & Morris (2020) wanaeleza kwamba data za msingi mara nyingi huitwa data ghafi, kwani bado hazijapitia mchakato wa uchambuzi au kazi nyingine. Data za msingi zilipatikana kupitia mbinu za ushuhudiaji na usaili. Data hizi zilishiriki katika uchambuzi wa athari za kifonolojia za lugha ya Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera

#### 3.6.2 Data za Upili

Data za upili ni data ambazo tayari zimekusanywa na watafiti wengine kwa malengo yao ya utafiti. Data hizi hutumiwa kuongeza na kuboresha data za msingi ili kutoa mchango mpya katika utafiti unaofanywa (Mat-Roni na wenzake, whj). Data za upili zinaweza kupatikana kutoka kwa vyanzo mbalimbali kama vitabu, makala, tasnifu za uzamili na uzamivu, magazeti, na makala zilizoko kwenye tovuti na wavuti. Kwa hiyo, data za upili zilikusanywa kupitia mbinu ya uchanganuzi wa matini.

Hivyo basi, data hizi zilikuwa muhimu katika ubainishaji wa mikakati ya kukabili athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

### 3.7 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti ni zana na vifaa vyote vinavyotumika katika mchakato wa ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti kutoka mwanzo hadi mwisho (Majid, khj). Kwa hiyo, vifaa vilivyotumiwa katika utafiti wetu ni pamoja na mwongozo wa ushuhudiaji, mwongozo wa usaili,

mwongozo wa uchanganuzi matini, kalamu, penseli, karatasi, madaftari, kompyuta, simu za mkononi na saa.

### 3.8 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ni mchakato wa kuchambua data zilizokusanywa, kuzipanga katika makundi husika na kuziwasilisha kulingana na malengo ya utafiti (Corbin& Anselm, 2009). Katika utafiti tuliofanya, data zilichanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli.

Mkabala huu unahusisha maelezo zaidi wakati wa kuchambua data kuliko takwimu (Corbin& Anselm, whj). Kutokana na utafiti wetu kuwa wa kitaamuli, data za utafiti zilichanganuliwa kwa kutumia madondoo na maelezo.

### 3.9 Itikeli za Utafiti

Rana, Dilshad & Ahsan (2021) wanasema kwamba, itikeli ya utafiti ni msingi muhimu wa utafiti ambao hufafanua maadili na mtazamo wa mtafiti kuhusu haki, thamani na hadhi ya washiriki wake. Katika kuhakikisha itikeli ya utafiti, mtafiti alichukua hatua kadhaa. Kwanza, alitafuta idhini kabla ya kukusanya data kutoka kwa Chuo cha Rwanda na kwa wilaya ya Bugesera. Pili, alitumia washiriki waliokuwa tayari kushiriki kwa hiyari. Tatu, washiriki ambao hawakutaka majina yao yatangazwe kwenye utafiti, majina yao yalihifadhiwa. Hivyo basi, itikeli hizi zilihakikisha kuwa utafiti unafanyika kwa heshima na uadilifu na kutodhuru washiriki wake.

### 3.10 Uhalali na Uthabiti wa Utafiti

Uhalali ni moja ya mbinu za utafiti wa kitamuli ambayo unategemea kuhakikisha ikiwa matokeo ya utafiti ni sahihi kutokana na malengo ya utafiti (Arslan, 2022). Arslan (khj) wanasema pia kwamba uhalali wa utafiti huhusisha dhana tofauti ambazo ni pamoja na uaminifu, uhalisia na uaminikaji.  Aidha, kulingana na Arslan (khj), uthabiti wa utafiti ni jinsi ya kuaminika, kukubalika na kurudia matokeo ya utafiti, ukionesha uhakika wa matokeo na uwezekano wa kujirudia katika mazingira tofauti. Kwa lengo la kuhakikisha uhalali na uthabiti wa utafiti, mbinu za hapo chini zilizingatiwa.

Kwanza kabisa, kabla ya kuanza utafiti, mtafiti alieleza kwa washiriki malengo na umuhimu wa utafiti. Pili, mtafiti alijaribu kutumia lugha rahisi ili aweze kuelewana na washiriki wa utafiti kwa urahisi. Tatu, mtafiti alitumia njia mseto inayopunguza hatari ya makosa ya utafiti yanayoweza

kujitokeza kutokana na mtafiti au washiriki wa utafiti. Mwishowe, mtafiti alijitahidi kuepuka kubadilisha taarifa zilizopatikana wakati wa ukusanyaji wa data.

### 3.11 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura ya tatu imeshughulikia methodolojia ya utafiti. Kwa hiyo, imezingatia utangulizi, paradima ya utafiti, usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango, sampuli, mbinu za kukusanyia data, aina za data, vifaa vya utafiti, uchambuzi wa data, uhalali na uthabiti na muhtasari wa sura ya tatu.

# SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.0 Utangulizi

Sura ya nne inahusu uwasilishaji na mjadala waa matokeo ya utafiti. Kwa hiyo, sura hii inagawanyika katika sehemu nne. Sehemu hizo ni utangulizi, athari za kifonolojia za lugha ya Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili, mikakati ya kukabili athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili na muhtasari.

## 4.1 Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Ujifunzaji wa Kiswahili

Utafiti uliofanyika ulikusudia kutimiza lengo mahususi la kwanza la kubainisha athari za kifonolojia za lugha ya Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Ili kutimiza lengo hili, mtafiti alichambua matini za watafiti tofauti ili kujua athari za kifonolojia katika ujifunzaji wa Kinyarwanda. Pili, mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano na walimu. Tatu, mtafiti alifanya ushuhudiaji ili kupata taarifa halisi kuhusu athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari katika wilaya ya Bugesera na sababu za athari hizo.

Zaidi ya hayo, uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti umeongozwa na mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi. Mhimili husika unasisitiza kuwa, sababu kuu ya matatizo na makosa katika kujifunza lugha ya pili ni athari za lugha ya kwanza. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule katika wilaya ya Bugesera zinajitokeza katika irabu na katika Konsonanti. Hivyo basi, sehemu husika inagawanyika katika sehemu tatu ambazo ni pamoja na athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika irabu, athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika konsonanti na athari za kifonolojia za mpangilio mbaya wa fonimu katika maneno.

### 4.1.1 Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Irabu

Kwa mujibu wa Massamba (2011), katika michakato ya kimofofonolojia kuna uwezekano kuwa fonimu fulani zinaweza kuathiriwa kwa namna fulani katika lugha fulani. Matokeo ya utafiti uliofanyika yameonesha kwamba kuna athari za kifonolojia za Kinyarwanda zinazoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa fonimu za irabu.

Athari hizo zimegawanyika katika makundi matatu: uchopekaji, udondoshaji, na ubadilishaji wa irabu. Kwa kubainisha athari hizi, tumelinganisha lugha ya Kinyarwanda na ya Kiswahili. Mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi unasisitiza kuwa sababu kuu ya matatizo na makosa katika kujifunza lugha ya pili ni athari za lugha ya kwanza. Kulingana na Kanake & Kobia (2023), mhimili husika unaonesha kuwa kulinganisha lugha hizo mbili hutumika kutabiri matatizo na makosa ambayo yatajitokeza wakati wa kujifunza lugha ya pili.

#### 4.1.1.1 Uchopekaji wa Irabu

Uchopekaji ni hali ya kifonolojia inayohusisha kuongeza kipashio katika neno. Matokeo ya hali hii ni kuunda neno ambalo lina sauti ya ziada ambayo haikuwapo katika neno asili (Wanjala, Mukoyani & Agaba, 2023). Katika utafiti uliofanyika, uchopekaji wa irabu umedhihirishwa kama mojawapo ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda ambazo zinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Bugesera.

Data za ushuhudiaji na uchambuzi wa nyaraka za wanafunzi zinadhihirisha kwamba wanafunzi wanachopeka irabu wanapoandika na kuzungumza Kiswahili. Mifano ifuatayo inaonesha wazi shida hiyo.

| **(1)** | **Kiswahili chenye Makosa** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|
| (a) | *Mubu* | *Mbu* |
| (b) | *Inne* | *Nne* |
| (c) | *Umbwa* | *Mbwa* |
| (d) | *Muntu* | *Mtu* |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na data hizi, tunaona namna athari ya uchopekaji wa irabu kutoka Kinyarwanda inavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Bugesera. Katika mfano (a), irabu “u” inachopekwa katika neno "mbu"kuwa "mubu." Katika mfano (b), "nne" irabu “i”inachopekewa katika neno nne na kuwa "inne." Katika mfano (c), "mbwa" irabu “I” inachopekewa katika neno mbwa na kuwa "umbwa." Katika mfano (d), neno "mtu" irabu u inachopekwa na kuwa "mutu.

Hii inaonesha kwamba wanafunzi wa Kinyarwanda wanapojifunza Kiswahili wanaathiriwa na uchopekaji wa irabu, kama ilivyo katika maneno ya Kinyarwanda, jambo ambalo linaathiri

uwezo wao wa kutumia Kiswahili sanifu. Makosa haya ya kimatamshi na kimaandishi yanaonesha umuhimu wa kuelewa athari za lugha ya kwanza (Kinyarwanda) katika ujifunzaji wa lugha ya pili (Kiswahili), ili kuboresha ujifunzaji na mawasiliano kwa Kiswahili sanifu.

Aidha, data za mahojiano na baadhi ya walimu wa Kiswahili zinabainisha kwamba uchopekaji wa irabu ni mojawapo ya athari za kifonolojia ya Kinyarwanda ambazo zinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili. Dondoo lifuatalo linaeleza:

> Mojawapo ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda zinazoathiri wanafunzi kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili kwenye shule hii ni uchopekaji wa irabu kwa maneno ya Kiswahili. Wanafunzi wetu wanatabia ya kuongeza sauti ya "u" au "i" kwenye maneno ya Kiswahili. Kwa mfano, badala ya kuandika "mtu" wanaandika "mutu". Pengine, badala ya kuandika "nne", wanaandika "inne". Athari hii hupatikana hasa katika maandishi na inaathiri vibaya ujifunzaji wa Kiswahili (mwalimu 2).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na data hizi, inaonekana kwamba athari mojawapo ya kifonolojia ya Kinyarwanda kwa wanafunzi katika kujifunza Kiswahili ni kuongeza sauti ya "u" au "i" kwenye maneno. Hii husababisha matatizo katika uandishi wa Kiswahili, ikionesha changamoto kubwa katika ujifunzaji wao. Hivyo basi, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba uchopekaji wa irabu ni mojawapo wa athari za kifonolojia za Kinyarwanda zinazoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

Katika kujadili athari za uchopekaji wa irabu, tafiti nyingine zinaonesha kwamba hali hii inaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa mchakato wa kujifunza lugha, hasa pale ambapo wanafunzi wanapokabiliwa na mazingira ya lugha mbili. Kwa mfano, tafiti za Wanjala, Mukoyani, na Agaba (2023) zinabaini kuwa uchopekaji wa irabu unaweza kupelekea matatizo ya matamshi na maandiko, na hivyo kuathiri ufahamu wa lugha mpya.

Utafiti wa Okwiri (2022) pia unaonesha kwamba wanafunzi wanaotoka kwenye mazingira ya lugha ya Kinyarwanda mara nyingi wanakumbana na changamoto kama hizi, ambapo wanatumia uchopekaji kuhamasisha sauti za Kinyarwanda katika lugha ya Kiswahili. Hii inadhihirisha kwamba uchopekaji wa irabu unaleta mabadiliko katika mfumo wa kifonolojia, na kwamba ni muhimu kwa walimu na watafiti kuzingatia hali hii ili kuboresha mbinu za ufundishaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wanaotoka katika maeneo ya Kinyarwanda.

#### 4.1.1.2 Udondoshaji wa Irabu

Udondoshaji ni hali ya kuondoa kipashio katika neno kwa namna inayokiuka taratibu za lugha husika (Wanjala, Mukoyani & Agaba, 2023). Aidha, katika fonolojia, udondoshaji wa irabu ni hali inayotokea iwapo irabu fulani inaondolewa kwenye neno kwa kukiuka sharia za lugha hiyo. Matini tofauti ambazo tulizichanganua kama vile Ontieri (2017) na Ontieri (2010), zimeonesha kwamba athari ya udondoshaji inayoathiri ujifunzaji wa Kiswahili ni udondoshaji wa konsonanti. Tofauti na haya, matokeo ya utafiti wetu yameonesha kwamba udondoshaji wa irabu ni mojawapo wa athari za kifonolojia za Kinyarwanda ambazo huathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Hii inathibitishwa na matokeo ya data za mahojiano na walimu wa Kiswahili kama inavyodhihiriks katika dondoo hili.

> Athari nyingine ya kifonolojia ya Kinyarwanda ambayo inawaathiri wanafunzi wetu kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili ni kutoa irabu kwenye maneno ya Kiswahili. Kuna baadhi ya maneno ya Kiswahili ambayo yanawatatiza wanafunzi wetu kuyaandika au kuyatamka. Kwa kuwa katika Kinyarwanda, irabu mbili hazifuatani, wanafunzi wanapoandika maneno ya Kiswahili hasa ambapo irabu mbili sawa zinafuatana, wanaandika moja na kuacha nyingine. Jambo hili huathiri matumizi yao ya Kiswahili fasaha na linaathiri ujifunzaji wao wa Kiswahili (mwalimu, 4).
>
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Hapa tunaona kwamba athari nyingine ya fonolojia ya Kinyarwanda kwa wanafunzi katika kujifunza Kiswahili ni kwamba wanafunzi wanashindwa kutamka na kuandika maneno yenye irabu mbili zinazofuata kwa usahihi. Kwa kuwa Kinyarwanda hakina irabu mbili zinazofuatana, wanafunzi huacha moja na kuandika nyingine pekee, jambo linaloathiri ufasaha wao katika Kiswahili. Vilevile,data za ushuhudiaji na uchambuzi wa nyaraka za wanafunzi zimedhihirisha kwamba wanafunzi wanafanya udondoshaji wa irabu wanapoandika na kuzungumza Kiswahili. Hii inaweza kuathiri ufasaha wao na mchakato wao wa kujifunza Kiswahili. Hii ni baadhi ya mifano inayoonesha changamoto hii.

| **(2)** | **Kiswahili chenye Makosa** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|
| (a) | *Sa* | *Saa* |
| (b) | *Muze* | *Mzee* |
| (c) | *Kunga* | *Kuunga* |
| (d) | *Koga* | *Kuoga* |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kwa mujibu wa tafsiri ya jedwali hili, wanafunzi wa Kiswahili kwenye shule za sekondari katika wilaya ya Bugesera wanakumbwa na changamoto za kutamka na kuandika maneno kwa usahihi kutokana na athari ya Kinyarwanda, ambapo irabu mbili haziwezi kufuatana. Kwa mfano, wanafunzi huandika "sa" badala ya "saa." Udondoshaji huu unatokana na kwamba katika Kinyarwanda hairuhusiwi kufuatanisha irabu mbili. Hali hii pia inajitokeza kwenye neno "mzee," ambapo wanafunzi wanatumia "muze" badala ya "mzee" sahihi kwa Kiswahili. Aidha, wanafunzi wanatumia "kunga" badala ya "kuunga." Udondoshaji huu unasababishwa na kwamba katika Kinyarwanda neno "kuunga" linatumiwa kama "kunga," jambo linalowafanya wanafunzi kuacha irabu moja wakati wa kutamka au kuandika Kiswahili.

Pia, udondoshaji wa irabu ulidhihirika kwenye neno "kuoga," ambapo kwa kuwa katika Kinyarwanda wanasema "koga," wanafunzi wanataka kutumia neno hili kama linavyotumika kwa Kinyarwanda, jambo linaloathiri ujifunzaji wao wa Kiswahili. Hali hii inawaathiri wanafunzi na kuwasababisha kudondosha irabu moja, hivyo kuzalisha maneno ambayo si ya Kiswahili sanifu. Kwa hiyo, udondoshaji wa irabu ni mojawapo ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda ambazo zinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera, nchini Rwanda.

Katika utafiti wetu, tuliona kwamba udondoshaji wa irabu ni tatizo kubwa linalowakabili wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Bugesera katika mchakato wa kujifunza Kiswahili. Hali hii haikupishana na matokeo ya tafiti zilizofanyika awali na watafiti wengine. Kwa mfano, tafiti za Ontieri (2010) na Ontieri (2017) zimedhihirisha kwamba udondoshaji wa konsonanti unawaathiri wanafunzi katika mchakato wa kujifunza lugha mpya. Hata hivyo, utafiti wetu umefichua kwamba udondoshaji wa irabu pia ni tatizo kubwa miongoni mwa wanafunzi wa Kinyarwanda wanapojifunza Kiswahili, jambo ambalo linaungwa mkono na ripoti kutoka kwa walimu na uchanganuzi wa maandiko ya wanafunzi.

Kulingana na data zilizokusanywa, wanafunzi wanakumbwa na changamoto ya kuondoa irabu mbili zinazofuata, jambo ambalo linatokana na muundo wa fonolojia wa Kinyarwanda ambapo irabu hizo haziwezi kuwepo kwa pamoja. Hii ni mifano halisi wa jinsi mazingira ya lugha yanavyoathiri ujifunzaji wa lugha mpya, kama ilivyoelezwa na Wanjala, Mukoyani, na Agaba (2023), ambao wamesisitiza umuhimu wa kuelewa vikwazo vya kifonolojia katika mchakato wa

kujifunza lugha. Hivyo, athari ya udondoshaji wa irabu inathibitisha kuwa ni muhimu kuzingatia hali hizi ili kuboresha mbinu za ufundishaji na kujifunza Kiswahili, kama ilivyoainishwa katika tafiti zilizopita.

#### 4.1.1.3 Ubadilishaji wa Irabu

Ubadilishaji ni hali inayotokea iwapo, fonimu moja inabadilishwa na nyingine kimakosa kwenye neno. Wanjala na wenzake (2023). Mukashyaka (2023), wanaonesha kwamba, mojawapo ya athari za kifonolojia za lugha za kibantu katika ujifunzaji wa Kiswahili, ni ubadilishaji wa fonimu. Matokeo ya utafiti wa watafiti hawa yanaonesha kwamba, fonimu zinazobadilishwa ni konsonanti. Licha ya haya, matokeo ya utafiti wetu yameonesha kwamba ubadilishaji wa irabu ni athari ya kifonolojia ya Kinyarwanda ambayo inaweza kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Athari hii imethibitisha na data zilizotolewa na walimu wa Kiswahili walioshiriki katika utafiti huu. Hili ni dondoo la mmojawapo wa walimu hao:

> Mojawapo ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzai wa Kiswahili katika shule ya sekondari hii ni kuchanganya sauti za Kinyarwanda na za Kiswahili. Pengine, wanafunzi wetu, kwa kuathiriwa na Kinyarwanda kuna maneno ambayo wanayaandika vibaya kwa kuathiriwa na Kinyarwanda. Kwa mfano, wanaandika “tanu” badala ya “tano” au “safuria” badala ya “sufuria”. Huku kuchanganya irabu kuaathiri sana ujifunzaji wa Kiswahili kwa wnafunzi wetu (mwalimu, 5)
>
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na dondoo hili tunaona kwamba athari za kifonolojia za Kinyarwanda zinawaathiri wanafunzi wa Kiswahili katika shule ya sekondari kwa kuchanganya sauti za Kinyarwanda na za Kiswahili. Wanafunzi wanaandika maneno kama "tanu" badala ya "tano" na "safuria" badala ya "sufuria," jambo ambalo linakwamisha ufasaha wao katika Kiswahili.Aidha, data za ushuhudiaji na uchambuzi wa nyaraka ulidhihirisha changamoto hii. Mifano ifuatayo inathibitisha changamoto hii:

| **(3)** | **Kiswahili chenye Makosa** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|
| (a) | *Tanu* | *Tano* |
| (b) | *Mcheli* | *Mchele* |
| (c) | *Safuria* | *Sufuria* |
| (d) | *Sabune* | *Sabuni* |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kutokana na datahizi , wanafunzi wa Kiswahili kwenye shule za sekondari teule katika wilaya ya Bugesera wanakumbwa na athari ya kubadilisha irabu kutokana na ushawishi wa Kinyarwanda. Kwa mfano, wanaandika "tanu" badala ya "tano." Hii ni kwa sababu, katika Kinyarwanda, neno hili linaandikwa kama "gatanu," jambo linaloathiri wanafunzi na kuwasababisha kubadilisha irabu ya mwisho.

Pia, wanatumia "mcheli" badala ya "mchele." Chanzo cha athari hii ni kwamba katika Kinyarwanda neno hili linaandikwa kama "umucheri," hivyo wanafunzi wanafanya kosa la kubadilisha irabu wakati wa kutumia neno hili kwa Kiswahili. Aidha, wanafunzi wanatumia "safuria" badala ya "sufuria." Chanzo cha ubadilishaji huu ni kwamba katika Kinyarwanda wanatumia "isafiriya," jambo linalowafanya wanafunzi kubadilisha irabu na kuzalisha neno lisilo sahihi kwa Kiswahili.

Mwisho, data zimeonesha kwamba wanafunzi wanatumia "sabune" badala ya "sabuni." Hii ni kwa sababu katika Kinyarwanda kuna neno "isabune," na hivyo wanafunzi wanabadilisha irabu katika neno hili, jambo linaloathiri ufasaha wao wa Kiswahili. Kwa hiyo, ubadilishaji wa irabu huathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

Katika utafiti wetu, tumegundua kwamba ubadilishaji wa irabu ni tatizo linalowakabili wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Bugesera katika mchakato wa kujifunza Kiswahili. Hali hii inaunga mkono matokeo ya tafiti zilizofanywa na Wanjala na wenzake (2023) na Mukashyaka (2023), ambao pia walibaini kwamba ubadilishaji wa fonimu, hasa konsonanti, ni tatizo linalohusiana na athari za kifonolojia za lugha za kibantu. Hata hivyo, utafiti wetu umeonesha kwamba ubadilishaji wa irabu ni changamoto kubwa katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi hawa.

Hivyo basi, walimu wa Kiswahili wanapaswakujenga mbinu bora za ufundishaji zinazoweza kushughulikia matatizo haya ya kifonolojia ili kuboresha uelewa na ujuzi wa wanafunzi katika Kiswahili. Utafiti wetu umeonesha kwamba kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia tofauti za kifonolojia ni hatua muhimu katika kusaidia wanafunzi kufikia ufasaha katika Kiswahili.

### 4.2 Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Konsonanti

Kwa mujibu wa Massamba (2011), katika michakato ya kimofofonolojia kuna uwezekano kuwa fonimu fulani zinaweza kuathiriwa kwa namna fulani katika lugha fulani. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba kuna athari za kifonolojia za Kinyarwanda zinazoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa fonimu za irabu. Athari hizo zimegawanyika katika makundi matatu: uchopekaji, udondoshaji, na ubadilishaji wa irabu.

#### 4.2.1 Athari ya Uchopekaji wa Konsonanti

Uchopekaji wa konsonani ni hali ya kuongeza konsonanti kwenye neno kimakosa na kuzalisha neon jingine ambalo halimo katika lugha husika. Utafiti uliofanywa na Ngugi (2017) unaonesha kwamba ujifunzaji wa Kiswahili unaathiri na athari za kifonolojia za lugha za Kibantu. Kwa kuchukua mfano wa Kisamia, mtafiti huyu anaonesha kwamba wanafunzi ambao Kisamia ni lugha yao ya kwanza, wanaathariwa na athari na Kisamia kiasi kwamba wanaongeza konsonanti za ziada kwenye maneno ya Kiswahili. Mifano ifuatayo inadhihirisha hili:

| **(4)** | **Kiswahili cha Wasamia** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|
| (a) | ***M**bumuazi* | *Bumbuazi* |
| (b) | ***N**janga* | *Janga* |
| (c) | *Umewa**n**dia* | *Umewadia* |
| (d) | ***N**dukani* | *Dukani* |
| (e) | *U**n**chaguzi* | *Uchaguzi* |
| (f) | *Sa**m**buni* | *Sabuni* |

**Chanzo**: Ngugi (2007:44)

Kulingana na data hizi, inaonekana kwamba, wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kisamia wanachopeka konsonanti wanapojifunza Kiswahili. Kwa mfano, wanaandika "mbumbuazi" badala ya "bumbuazi," "njanga" badala ya "janga," na "umewandia" badala ya "umewadia". Aidha, wanaandika "ndukani" badala ya "dukani," "unchaguzi" badala ya "Uchaguzi," na "sumbuni" badala ya "sabuni."

Hii inaonesha jinsi mabadiliko ya konsonanti kutoka Kisamia yanavyoathiri matamshi na maandiko yao katika Kiswahili. Aidha, matokeo ya utafiti kutoka kwa mahojiano na walimu wa Kiswahili yanaonesha kwamba uchopekaji wa konsonanti ni mojawapo ya athari za kifonolojia

za Kinyarwanda ambazo zinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili wilayani Bugesera. Mmojawapo wa walimu alieleza hili katika dondoo lifuatalo:

> Athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule yetu ni kwamba wanafunzi wanazungumza Kiswahili na kukiandika kama Kinyarwanda. Hii inapelekea maneno ya Kiswahili kuwa na sauti zisizohitajika, ambazo ni za ziada (mwalimu 1).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kotokana na data hizi, tunaona kwamba, wanafunzi wanaathiriwa na fonolojia ya Kinyarwanda kiasi kwamba wanaongeza fonimu za ziada kwenye maneno ya Kiswahili na kuzalisha maneno yasiyo ya Kiswahili sanifu. Haya yanayosemwa na mwalimu 1, yanathibitishwa na mwenzake ifuatavyo:

> Wanafunzi wetu, kwa kuathiriwa na fonolojia ya Kinyarwanda, wanaongeza konsonanti za ziada kwenye maneno ya Kiswahili. Hii husababisha matatizo katika uandishi na matamshi sahihi ya maneno ya Kiswahili. Athari hii inaathiri ujifunzaji wao wa Kiswahili kwa ujumla (mwalimu 4)
> . **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Data hizi zinamaanisha kwamba, fonolojia ya Kinyarwanda inasababisha wanafunzi kuongeza konsonanti za ziada kwenye maneno ya Kiswahili na kuathiri vibaya ujifunzaji wao wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu, kwa kuongeza konsonanti za ziada kwa maneno ya Kiswahili, wanaunda maneno mapya ambayo si ya Kiswahili sanifu.

Zaidi ya hayo, athari ya uchopekaji wa konsonanti katika ujifunzajiwa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari teule katika wilaya ya Bugesera ilidhihirika wakati wa ushuhudiaji na uchambuzi wa nyaraka za wanafunzi.

Mtafiti alibaini kuwa uchopekaji wa konsonanti unaathiri wanafunzi, kwani ilionekana kwamba wanaongeza konsonanti kwenye baadhi ya maneno. Hii ni baadhi ya mifano inayoonesha uchopekaji wa konsonanti.

| **(5)** | **Kiswahili chenye Makosa** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|
| (a) | *Mntu* | *Mtu* |
| (b) | *Kunyamanza* | *Kunyamaza* |

**Chanzo**: data za Uwandani (2024)

Kutokana hizi , wanafunzi wa Kiswahili kwenye shule za sekondari teule katika wilaya ya Bugesera wanakumbwa na changamoto za matumizi sahihi ya maneno ya Kiswahili kutokana na athari ya lugha ya Kinyarwanda. Kwa mfano, neno "mntu" limetumika badala ya "mtu."

Pia, neno "kunyamanza" limetumika badala ya "kunyamaza." Athari hii inatokana na lugha ya Kinyarwanda ambapo kuna uwezekano wa maneno yenye asili ya kufanana kutumika vibaya katika Kiswahili. Hivyo wanafunzi wanachanganya maneno yasiyo na uhusiano wa moja kwa moja na maana sahihi katika Kiswahili. Makosa haya yanaathiri ufasaha wa wanafunzi katika kujifunza na kutumia Kiswahili sanifu. Kwa hiyo, matokeo ya utafiti uliofanyika yanaonesha kwamba uchopekaji ni mojawapo ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda zinazoathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

Matokeo ya utafiti wetu yanaendana na tafiti zilizotangulia, kama ilivyoonesha utafiti wa Ngugi (2017) kuhusu athari za kifonolojia za lugha za Kibantu kwenye ujifunzaji wa Kiswahili. Hii ina maana kwamba wanafunzi wa Kiswahili, haswa wale wanaotoka katika mazingira ya Kinyarwanda, wanakumbwa na changamoto za fonolojia ambazo zinawazuia kujifunza Kiswahili kwa ufanisi. Utafiti wetu umebaini kwamba uchopekaji wa konsonanti unachangia katika kuunda maneno yasiyo ya Kiswahili sanifu, hali inayothibitisha matokeo ya watafiti wengine. Umahususi wa utafiti wetu unalenga athari za Kinyarwanda kwenye ujifunzaji wa Kiswahili wilayani Bugesera, ambapo mazingira ya lugha na utamaduni yanaweza kuathiri mchakato wa kujifunza lugha mpya. Hivyo, matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa kuelewa namna ambavyo lugha ya nyumbani inaweza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili, na inasisitiza haja ya kuzingatia muktadha wa kijamii na lugha katika kufundisha Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

### 4.2.2 Athari ya Udondoshaji wa Konsonanti

Udondoshaji ni hali ya kuondoa kipashio katika neno kwa namna inayokiuka taratibu za lugha husika (Wanjala, Mukoyani & Agaba, 2023). Katika utafiti uliofanyika, udondoshaji umedhihirishwa kama mojawapo ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda ambazo zinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

Kwanza, data kutoka uchanganuzi matini za tafiti tangulizi zimeonesha kwamba, kuna athari za kifonolojia za lugha za Kibantu katika ujifunzaji wa Kiswahili. Hii inathibitisha na matokeo ya utafiti wa Ontieri (2010), akionesha kwamba udondoshaji ni mojawapo ya athari ya kifonoloji za lugha ya kwanza ambazo zinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nakuru, nchini Kenya. Athari hii inathibitishwa na jedwali lifuatalo:

| (6) | **Udondoshaji** | **Sahihi** |
|---|---|---|
| *(a)* | *g^mu* | *Ghamu* |
| *(b)* | *kus^takiwa* | *Kushtakiwa* |
| *(c)* | *majo^zi* | *majonzi* |
| *(d)* | *ukwe^si* | *Ukwensi* |
| *(e)* | *kuvu^jamoyo* | *kuvunja moyo* |

**Chanzo**: Ontieri (2010:50)

Kutokana na data hizi, tunaona kwamba udondoshaji wa konsonanti unaathiriwa ujifunzaji wa Kiswahili kwanza kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nakuru, Kenya. Wao wanaandika na kutamka "majo^zi" badala ya "majonzi", "ukwe^si" badala ya "ukwensi", "kus^takiwa" badala ya "kushtakiwa", "g^mu" badala ya "ghamu", na "kuvu^jamoyo" badala ya "kuvunja moyo".

Hii inathibitisha matokeo ya Ontieri kwamba athari za kifonolojia za lugha ya kwanza husababisha udondoshaji wa konsonanti, na kuathiri jinsi wanafunzi wanavyopokea na kutumia maneno ya Kiswahili. Aidha, mahojiano na walimu walioshiriki kwenye utafiti wetu wamethibitisha kwamba udondoshaji wa konsonanti ni mojawapo ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda ambazo huathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Bugesera. Huyu ni mmojawapo wa walimu wa Kiswahili waliohojiwa

> Athari za kifonolojia za Kinyarwanda zinazokwamisha ujifunzaji wa Kiswahili katika shule hii ni nyingi. Moja ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda inayowaathiri wanafunzi wetu ni kuondoa baadhi ya sauti kutoka kwenye maneno ya Kiswahili. Wanafunzi wanapojaribu kusema au kuandika baadhi ya maneno ya Kiswahili, wanapunguza baadhi ya konsonanti kwa kuandika maneno hayo kwa mtindo wa Kinyarwanda. Kwa kufanya makosa haya, wanaandika maneno yasiyo ya Kiswahili. Athari hii inakwamisha ujifunzaji wao wa Kiswahili kwa sababu inawazuia kuandika na kuzungumza Kiswahili kwa usahihi (mwalimu,7)
> . **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Mwalimu huyu anaonesha kwamba, wanafunzi wanapoandika au wanaposema maneno ya Kiswahili wanaondosha baadhi ya konsonanti kwa kuathiriwa na fonolojia ya Kinywarwanda. Vilevile, athari ya udondoshaji wa konsonanti kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari teule katika wilaya ya Bugesera ilidhihirika wakati wa ushuhudiaji na uchambuzi wa nyaraka za wanafunzi hasa notisi na kazi za ujifunzaji wanazofanya kimaandishi Haya ni baadi ya makosa yanayofanywa na wanafunzi kutokana na udondoshaji wa konsonanti

| **(7)** | **Kiswahili chenye Makosa** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|
| (a) | *Ne* | *Nne* |
| (b) | *Imbo* | *Nyimbo* |
| (c) | *Imbo* | *Wimbo* |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2024)

Kutokana na datahizi, wanafunzi wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera wanakabiliwa na changamoto za kutamka na kuandika maneno sahihi kutokana na athari ya lugha ya Kinyarwanda. Kwa mfano, neno "ne" limetumika badala ya "nne." Hii inatokana na athari ya lugha ya Kinyarwanda ambapo neno "ne" hutumika kumaanisha "nne," hivyo wanafunzi wanachanganya matamshi na kufupisha neno la Kiswahili, na kusababisha makosa.

Vilevile, neno "imbo" limetumika badala ya "nyimbo" na pia imbo badala ya "wimbo." Hii inatokana na Kinyarwanda ambapo neno "indirimbo" hutumika kwa maana ya "wimbo" au "nyimbo". Wanafunzi wanapunguza baadhi ya sauti au kubadilisha matamshi katika Kiswahili.

Makosa haya yanaathiri ufasaha wa wanafunzi katika Kiswahili na uwezo wao wa kutumia maneno sahihi katika muktadha wa lugha. Kwa hiyo, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba udondoshaji wa konsonanti ni athari ya kifonolojia ya kinyarwanda inayoathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Hivyo basi, wakati wa ufundishaji wa Kiswahili, walimu wanalazimika kuzingatia mikakati ya kuepukana na athari hii kwa mafanikio ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

Matokeo ya utafiti wetu yanaendana kwa karibu na tafiti zilizotangulia, ambazo pia zimeonesha athari za kifonolojia za lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa Kiswahili. Kwa mfano, utafiti wa Ontieri (2010) umeonesha udondoshaji wa konsonanti kama kikwazo kwa wanafunzi wa shule za

sekondari katika wilaya ya Nakuru, Kenya. Hali hii inaonesha kuwa tatizo la udondoshaji wa konsonanti siyo la kipekee kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Bugesera bali ni tatizo pana linaloathiri wanafunzi katika maeneo mbalimbali ya Afrika Mashariki ambapo Kiswahili kinajifunzwa kama lugha ya pili.

Umahususi wa utafiti wetu unathibitishwa na ukweli kwamba umeangazia athari za kifonolojia za Kinyarwanda, lugha ya mama ya wanafunzi wetu, kwenye muktadha wa wilaya ya Bugesera. Utafiti wetu umetoa mchango muhimu katika kuelewa jinsi muktadha wa lugha ya kwanza unavyoweza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya pili, na hivyo kuwezesha walimu kuandaa mikakati ya kufundisha inayozingatia changamoto hizi. Kwa kuzingatia matokeo haya, ni muhimu kwa walimu kuunda mazingira ya kujifunza yanayosaidia wanafunzi kupunguza athari hasi za udondoshaji, ili kuboresha uelewa na ufanisi wao katika matumizi ya Kiswahili.

### 4.2.3 Athari ya Ubadilishaji wa Konsonanti

Ubadilishaji ni hali inayotokea iwapo, fonimu moja inabadilishwa na nyingine kimakosa kwenye neno. Kwa mujibu wa Wanjala na wenzake (2023)., ubadilishaji wa konsonanti ni mchakato ambapo konsonanti moja inabadilishwa na nyingine katika matumizi ya lugha.

Katika uchunguzaji wa athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule katika wilaya ya Bugesera, tumeona kwamba ubadilishaji wa konsonanti ni miongoni mwa athari hizi. Athari hii inathibitishwa na data zilizopatikana kwa kutumia uchanganuzi matini, mahojiano na ushuhudiaji.

Utafiti wa Ontieri (2017) unaonesha kwamba, wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kikisii wanaathiriwa na athari ya ubadilishaji wa konsonanti katika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Hili linadhihirishwa na mifano inayofuata:

| **(8)** | **Ubadilishaji** | **Sahihi** |
|---|---|---|
| *(a)* | *M**s**indo* | *M**sh**indo* |
| *(b)* | *Kushu**g**ulika* | *Kushu**gh**ulika* |
| *(c)* | *Anayechi**nchw**a* | *Anayechi**njw**a* |
| *(d)* | *Kilichohu**s**unisha* | *Kilichohu**z**unisha* |
| *(e)* | *Nikiwa**p**ungia* | *Nikiwa**b**ungia* |
| *(f)* | ***S**iwani* | ***Z**iwani* |

**Chanzo**: Ontieri (2017:9)

Data hizi zinaonesha jinsi wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kikisii wanavyoathiriwa na ubadilishaji wa konsonanti katika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Wanafunzi hawa wanaandika "msindo" badala ya "mshindo," "kushugulika" badala ya "kushughulika," na "anayechinchwa" badala ya "anayechinjwa." Aidha, wanaandika "kilichohusunisha" badala ya "kilichohuzunisha," "Nikiwapungia" badala ya "nikiwabungia," na "Siwani" badala ya "ziwani." Hii inaonesha jinsi mabadiliko ya konsonanti kutoka Kikisii yanavyoathiri matamshi na maandiko ya Kiswahili kwa wanafunzi hao, na hivyo kuathiri ufasaha wao katika lugha hiyo.

Aidha, utafiti wa Mukashyaka (2023) unaonesha kwamba ubadilishaji wa sauti ni athari ya Kinyarwanda ambayo inaathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari katika wilaya ya Nyanza nchini ya Rwanda. Mtafiti huyu anaonesha athari za ubadilishaji wa fonimu katika mifano ifuatayo:

| **(9)** | **Udondoshaji** | **Sahihi** |
|---|---|---|
| *(a)* | *Cura* | *Chura* |
| *(b)* | *Ngambo* | *ng'ambo* |
| *(c)* | *Temanini* | *Themanini* |
| *(d)* | *Zambi* | *Dhambi* |
| *(e)* | *Lambilambi* | *Rambirambi* |
| *(f)* | *Dirishya* | *Dirisha* |
| *(g)* | *Shyamba* | *Shamba* |

**Chanzo**: Mukashyaka (2023:37)

Data hizi zinaonesha kwamba wanafunzi hufanya makosa ya matamshi na kiotografia kwa sababu baadhi ya konsonanti za Kiswahili hazipo kwenye Kinyarwanda. Hivyo, wanafunzi wanapotamka au wanaponukuu maneno ya Kiswahili, wanatumia konsonanti za Kinyarwanda, na hivyo kuleta makosa kama vile "cura" badala ya "chura," "ngambo" badala ya "ng'ambo," na "temanini" badala ya "themanini." Aidha, wanaandika "zambi" badala ya "dhambi," "lambilambi" badala ya "rambirambi," na "dirishya" badala ya "dirisha." Hii inaonesha jinsi ubadilishaji wa sauti kutoka Kinyarwanda unavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi hao, huku wakipambana na changamoto za matamshi na maandiko sahihi.

Zaidi ya hayo, katika mahojiano tuliyofanya na walimu wa Kiswahili wilayani Bugesera, imebainika kwamba, wanafunzi wanaathiriwa na athari ya kubadilisha konsonanti kutokana na kuathiriwa na Kinyarwanda. Haya ni maelezo ya mwalimu mmojawapo.

> Athari ya Kifonolojia ya Kinyarwanda inayoathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule yetu ni kabadilisha sauti. Idadi kubwa ya wanafunzi wetu hawajui mahali pa kutumia sauti “l” na “r”. Hii ni kwa sababu, kwenye Kinyarwanda, sauti “l” inatumiwa mara chache. Athari hii inawasababisha kutumia “r” kwenye badala ya “l”. Kwa kufanya haya, wanaandika na kusema maneno yenye makosa (mwalimu,2).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kulingana na dondoo hili, athari za kifonolojia za Kinyarwanda zinazojitokeza kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule yetu ni mabadiliko ya sauti. Wanafunzi wengi wanapata shida kutofautisha na kutumia sauti “l” na “r” ipasavyo. Hii ni kwa sababu, katika lugha ya Kinyarwanda, sauti ya “l” hutumiwa mara chache. Athari hii inasababisha wanafunzi kutumia “r” badala ya “l,” na hivyo kuandika na kusema maneno kwa makosa. Mwalimu huyu aliungwa mkono mwa mwenzake akisema kwamba,

> Kuhusiana na athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujufunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule yetu, ni kutumia sauti za Kinyarwanda badala ya kutumia za Kiswahili. Kuna baadhi ya sauti zinazopatikana kwenye Kinyarwanda kama “shy” na “shyw” ambazo hazipo kwenye Kiswahili zinazotumiwa na wanafunzi wapoandika au wanapoongea Kiswahili (mwalimu,2).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili kwa wanafunzi wetu ni matumizi ya sauti za Kinyarwanda badala ya za Kiswahili, kama vile "shy" na "shyw". Wanafunzi wanachanganya sauti za lugha hizi mbili, na hivyo kushindwa kutumia sauti za Kiswahili ambazo hazipatikani kwenye Kinyarwanda. Maelezo ya mwalimu wa pili yanaungwa mkono na mwalimu mwenzake ifuatavyo:

> Sauti wanazozichanganya wanafunzi ni kama vile “dh”, “gh”, “ng’” na nyinginezo. Wanapotaka kuandika au kutamka sauti hizi kwenye mane, kuna wanafunzi ambao wanazitumia zile zianazopatikana kwenye Kinyarwanda badala ya kutumia sauti sahihi za Kiswahili. Hawa wanatumia “d” au “z” badala ya “dh”, “g” au “h” badala ya “gh” na “ng” badala ya “ng” (mwalimu,4).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Kulingana na dondoo hili, athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilikwa wanafunzi wetu ni kuchanganya sauti kama vile "dh," "gh," na "ng'." Wanafunzi wanapoandika au kutamka sauti hizi, wanatumia sauti za Kinyarwanda kama "d" au "z" badala ya "dh," "g" au "h" badala ya "gh," na "ng" badala ya "ng'." Aidha, wakati wa ushuhudiaji na

uchambuzi wa nyaraka za wanafunzi zimebainisha changamoto hii. Hii ni baadhi ya mifano ya ubadilishaji wa sauti iliyobainishwa kutoka kwa wanafunzi

| **(10)** | **Kiswahili chenye Makosa** | **Kiswahili Sanifu** |
|---|---|---|
| (a) | *Kurara* | *Kulala* |
| (b) | *Karamu* | *Kalamu* |
| (c) | *Cyayi* | *Chai* |
| (d) | *Dirishya* | *Dirisha* |
| (e) | *Zahabu* | *Dhahabu* |
| (g) | *Garama* | *Gharama* |

**Chanzo**: data za Uwandani (2024)

Kutokana na data zilizo katika jedwali hili, tunaweza kuona kwamba wanafunzi wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera wanakabiliwa na changamoto za kubadilisha sauti za maneno kutokana na ushawishi wa Kinyarwanda. Kwa mfano, neno "kurara" limetumika badala ya "kulala." Hii inatokana na kwamba katika Kinyarwanda neno la maana hiyo ni "kurara," hivyo wanafunzi wanachanganya na Kiswahili, na kusababisha kosa hilo. Vilevile, wanafunzi wanatumia "karamu" badala ya "kalamu." Huu ubadilishaji unatokana na ushawishi wa maneno yanayofanana katika lugha ya Kinyarwanda. Aidha, neno "cyayi" limetumika badala ya "chai," hali inayoonesha athari ya matamshi ya Kinyarwanda ambapo sauti ya "ch" inabadilishwa kuwa "cy."

Katika mfano wa neno "dirishya" badala ya "dirisha," wanafunzi wanaiga matamshi ya Kinyarwanda ambapo hutamka "dirishya." Vivyo hivyo, neno "zahabu" limeandikwa kama "dhahabu" kutokana na kosa la kubadilisha sauti za "z" na "dh" ambazo zinafanana kwa kiasi katika lugha hizi mbili. Neno "garama" badala ya "gharama" linaonesha ubadilishaji wa sauti ya "gh," ambapo wanafunzi wanaathiriwa na Kinyarwanda, hivyo wanatumia "g" badala ya "gh." Kwa ujumla, mabadiliko haya ya sauti ni athari za kifonolojia zinazoletwa na Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili, hali inayosababisha makosa katika matamshi na maandishi ya wanafunzi.

Mifano hii inaonesha jinsi mabadiliko ya konsonanti kutokana na athari za Kinyarwanda yanavyoathiri matamshi na maandiko yao katika Kiswahili, na hivyo kukwamisha ufasaha na uelewa wa wanafunzi katika lugha hiyo.

Kwa hiyo, walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari wanalazimika kufanya juu chini ili kuondoa athari zote za kifonolojia za Kinyarwanda ambazo zinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa shule za upili nchini  Rwanda.

Matokeo ya utafiti wetu yanaendana kwa karibu na matokeo ya tafiti zilizotangulia, hasa katika kuonesha jinsi athari za kifonolojia kutoka Kinyarwanda zinavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Utafiti wa Wanjala na wenzake (2023) na Mukashyaka (2023) umeonesha wazi kwamba ubadilishaji wa konsonanti ni tatizo kubwa kwa wanafunzi wa Kiswahili wenye asili ya Kinyarwanda na Kikisii. Vilevile, utafiti wetu umeonesha kwamba wanafunzi katika wilaya ya Bugesera wanakabiliwa na changamoto kama hizo, ambapo athari za lugha ya kwanza zinavyoathiri matamshi na maandiko yao. Umahususi wa utafiti wetu unatokana na utafiti wa kina uliofanyika katika wilaya ya Bugesera, ukilenga athari za Kinyarwanda kwenye ujifunzaji wa Kiswahili, na hivyo kuchangia katika ufahamu wa jinsi mazingira ya lugha yanavyoweza kuathiri mchakato wa kujifunza. Hii inadhihirisha umuhimu wa kufanya tafiti zaidi katika maeneo maalum ili kuelewa kwa undani changamoto zinazokabili wanafunzi katika kujifunza lugha mpya.

**4.23 Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Mpangilio Mbaya wa Fonimu**

Mpangilio wa mbaya wa fonimu katika maneno ni hali inayotokea iwapo irabu au konsonanti zimepangwa kwenye maneno kimakosa bila kufuata utaratibu wa kupanga maneno kwenye lugha husika. Katika utafiti uliofanyika, ilionekana kwamba mpangilio mbaya wa fonimu katika maneno ni mojawapo ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji waa Kiswahili kwenye shule za sekondari teule katika wilaya ya Bugesera nchini Rwanda. Ukweli huu ulithibitisha na data zilizopatikana kutoka uchanganuzi wa matini, mahojiano na ushuhudiaji.

Kwanza, utafiti wa Ntawiyanga (2015) unaonesha kwamba wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda wanaathiri na Kinyarwanda pale ambapo huweka mofu katika nafasi ambazo si sahihi kulingana na muundo wa lugha. Sababu kuu ya hali hii ni kutaka kuunda maneno kwa kufuata muundo wa lugha yao ya asili, Kinyarwanda. Aidha, mahojiano tuliyoyafanya na walimu yanathibitisha athari hii. Walimu wawili mingoni mwa walimu walioshiriki katika utafiti huu walithibitisha kuwa mpangilio mbaya wa fonimu katika maneno ni mojawapo ya athari za

kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili kwenye shule za sekondari. Dondoo lifuatalo linaeleza:

> Athari za kifonolojia ya Kinyarwanda ambayo inaathiri ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wetu, ni kupanga sauti za Kiswahili kama zinavyopangwa kwa lugha ya Kinyarwanda. Wanafunzi wanapozungumza au wanapoandika Kiswahili, inaonekana kwamba kwenye baadhi ya maneno wanapanga sauti vibaya kwenye maneno kutokana na kuzoea Kinyarwanda (mwalimu,6).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba athari za kifonolojia ya Kinyarwanda zinaonekana wazi kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili kwa wanafunzi wetu. Wanafunzi wanakabiliwa na changamoto ya kupanga sauti za Kiswahili kulingana na mazoea yao ya lugha ya Kinyarwanda. Hii inaonekana wanapozungumza au kuandika Kiswahili, ambapo mara nyingi wanapata shida katika mpangilio sahihi wa sauti katika maneno, kutokana na kuzoea mfumo wa Kinyarwanda. Mwalimu mwingine anaongezea kwamba

> Athari ya kifonolijia ya Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilikwa wanafunzi wetu, ni kuunda maneno kama wanavyounda maneno ya Kinyarwanda. Kwa kuathiriwa na Kinyarwanda, wanafunzi wetu wanapanga konsonanti na irabu vibaya kwenye maneno ya Kiswahili. Matokeo yanakuwa kwamba wanazalisha maneno mapya ambayo si ya Kiswahili sanifu. Kwa kweni, jambo hili linaathiri ujifunzaji wao wa Kiswahili (mwalimu, 5).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba athari ya kifonolojia ya Kinyarwanda ina athari kubwa kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilikwa wanafunzi wetu. Wanafunzi wanajaribu kuunda maneno ya Kiswahili kama wanavyounda maneno ya Kinyarwanda, na hivyo wanapanga konsonanti na irabu vibaya. Matokeo yake ni kwamba wanaweza kuzalisha maneno mapya ambayo si sahihi katika Kiswahili. Hii inaathiri ujifunzaji wao wa Kiswahili kwa kina na inahitaji mkakati wa kurekebisha ili kuboresha ustadi wao wa lugha. Aidha, data kutoka ushuhudiaji na uchambuzi wa nyaraka zinadhihirisha changamoto hii. Hii ni baadhi ya mifano kutoka ushuhudiaji na uchambuzi wa nyaraka

| **(11)** | **Kiswahili chenye makossa** | **Kiswahli Sanifu** |
|---|---|---|
| (a) | *Nilisomacho* | *nilichosoma* |
| (b) | *Anafundishaye* | *anayefundisha* |
| (c) | *Alifikapo* | *Alipofika* |
| (d) | *Nilionao* | *Nilioona* |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2024)

Data hizi zinaonesha kwamba, mpangilio mbaya wa fonimu una athari kubwa kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Wanafunzi wanapojifunza Kiswahili, mara nyingi wanapanga vibaya fonimu katika maneno, na hivyo kufanya makosa kama vile "nilisomacho" badala ya "nilichosoma," "anafundishaye" badala ya "anayefundisha," "alifikapo" badala ya "alipofika," na "nilionao" badala ya "nilioona."

Mpangilio huu mbaya wa fonimu unavuruga ufasaha wao wa lugha na kusababisha matatizo ya kuelewa na kutumia Kiswahili kwa usahihi. Hii inaonesha jinsi mabadiliko ya mpangilio wa fonimu yanavyoweza kupunguza uwezo wao wa kujieleza na kuandika katika Kiswahili.

Kwa kutaka kuelewa zababu zinazowasabisha wanafunzi kuathiriwa na fonolojia ya Kinyarwanda mpaka wakapanga fonimi kwenye maneno ya Kiswahili kama wanavyofanya kwa Kinyarwanda, matokeo ya utafiti yamebainisha sababu kuu mbili. Kwanza, mazingira ya nyumbani na ya shuleni hayawapi wanafunzi kuzungumza Kiswahili ili waweze kuepukanana na athari zi kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Kwenye mazingira ya nyumbani na shuleni, wanafunzi wanatumia Kinyarwanda tu.

Dondoo hili kutoa kwa mmojawapo wa walimu wa Kiswahili linaeleza sababu zinazowafanya wanafunzi kupanga fonimu vibaya kwenye maneno.

> Athari za kifonolojia za Kinyarwanda zinazoathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule hii zinasababishwa na mazingira ya nyumbani. Wanafunzi wanapotumia Kinyarwanda nyumbani, wanapata ugumu kubadilisha matamshi wanapokuwa shuleni wakijifunza Kiswahili. Ndiyo sababu wanapozungumza au wanapoandika Kiswahili huwa wanapanga vibaya sauti kwenye (mwalimu,2).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Athari za kifonolojia za Kinyarwanda zinazoathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule husika zinatokana na matumizi ya Kinyarwanda wakati mrefu ukilinganisha na Kiswahili. Aidha, wakati wa ushuhudiaji, ilidhihirika kwamba walimu wanapofundisha Kiswahili, wanatilia mkazo sarufi kuliko matamshi. Hii inaathiri wanafunzi kwa kuwa hawawezi kubobea katika fonolojia ya Kiswahili. Wanapokosa kuelewa na kutamka sauti za Kiswahili kwa usahihi, wanafunzi wanakumbwa na ugumu katika kuelewa maana na kutumia lugha kwa ufasaha.

Athari hii ni kubwa zaidi pale ambapo walimu hawazingatii umuhimu wa mafunzo ya kifonolojia, hali ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa kusababisha wanafunzi kupanga fonimu za Kiswahili kama wanavyozipanga kwenye maneno ya Kinyarwanda.

Zaidi ya hayo, wakati wa ushuhudiaji, ilionekana kwamba wanafunzi hawana mahali pa kuzungumzia Kiswahili. Kwenye shule ambapo ushuhudiaji ulifanyika, lugha inayotumika zaidi ni Kinyarwanda, na ni shule moja tu miongoni mwa zilizoshuhudiwa inayotumia Kiingereza katika shughuli zake zote. Hakuna shule yoyote inayotumia Kiswahili katika shughuli zote za shuleni miongoni mwa shule ambapo utafiti wetu ulifanyika.

Hii inamaanisha kuwa wanafunzi hawana fursa ya kutosha ya kujifunza na kutumia Kiswahili kwa vitendo, hali ambayo inaweza kuleta athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili. Kukosekana kwa matumizi ya Kiswahili katika mazingira ya kila siku kunapunguza uwezo wa wanafunzi kuzoea matamshi na sauti za lugha hiyo.

Kwa hiyo, matokeo yamebainisha sababu za athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwenye shule teule. Sababu ya kwanza ni changamoto za mazingira ya nyumbani ambapo Kinyarwanda kinatumika zaidi kuliko Kiswahili. Sababu ya pili ni, kusisitizia zaidi sarufi na fasihi kuliko fonolojia.

Kwa hiyo, ni lazima walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari teule katika wilaya ya Bugesera watumie mbinu za ufundishaji ambazo zitashiriki katika kuepukana na athari ya mpangilio mbaya wa fonimu katika maneno ya Kiswahili.

### 4.3 Mikakati ya Kukabili Athari ya Kifonolojia katika Kujifunza Kiswahili

Sahemu iliyotangulia imebainisha athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Kwa hiyo, sehemu hii inaangazia mikakati ya kukabili athari hizo. Ili kubabainisha mikakati hii, kwanza, tulifanya mahijiano na walimu wa Kiswahili. Mahojiano na walimu yaliongozwa na swali hili, *Je, ni mikakati gani unayotumia ili kukabili athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule hii*? Pili, tulifanya uchanganuzi matini.

Isitoshe, tulijiegemeza kwenye mhimili wa pili wa nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi. Mhimili huu unaonesha kuwa, unaonesha kuwa ili kukabili athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa

lugha ya pili, muhimu kufundisha wanafunzi kuhusu mifano ya mfanano kati ya lugha ya kwanza na ya pili. Jambo hili huwasaidia kujitambua na kuelewa ni wapi uhamishaji wao wa vipengele vya lugha ya kwanza hadi ya pili unafanikiwa na ni wapi haufanikiwi (Kanake Kanake & Kobia, 2023). Kwa hiyo sehemu inayofuata inazungumzia mikakati hiyo.

### 4.3.1 Kulinganisha Fonolojia ya Kinyarwanda na ya Kiswahili

Wakati wa ukusanyaji data kuhusu athari za kukabili athari za kifonolojia kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera, kulinganisha fonolojia ya lugha mbili kulibainishwa miongoni mwa mikakati mingine. Mkakati huu unadhihirishwa na mahojiano tuliyoyafanya na walimu. Hili ni jibu la mmojawapo wawalimu waliohojiwa.

> Mkakati wa kukabili athari za kifonolojia kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini kufundisha tofauti kati ya fonolojia za lugha mbili. Wanafunzi wanapojua tofauti za kifonolojia kati ya Kinyarwanda na Kiswahili Kwa kulinganisha fonolojia hizi mbili, wanafunzi wanaweza kuboresha matamshi yao ya Kiswahili. Hapa ni lazima walimu wafundishe fonolojia ya Kiswahili wakisisidizia zile sauti za Kiswahili ambazo hazipatikani kwenye lugha (mwalimu, 4)
> . **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba mkakati wa kukabiliana na athari za kifonolojia kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili ni kuwafundisha wanafunzi tofauti kati ya fonolojia za Kinyarwanda na Kiswahili. Kwa kulinganisha sauti za lugha hizi mbili, wanafunzi wanaweza kuboresha matamshi yao ya Kiswahili. Pia, wakati wa ufundishaji wa fonolojia ya Kiswahili, ni lazima kusisitizia zile zauti za Kiswahili ambazo hazipatikati kwa Kinyarwanda. Hoja hii iliungwa mkono na mwenzake ifuatavyo:

> Mkakati wa kukabili athari za kifonolojia kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini kuzingatia mafunzo ya fonolojia ya lugha zote mbili. Njia bora ya kushughulikia athari hizi ni kuwapa wanafunzi mafunzo maalum ya monolojia kwa lugha zote mbili. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wanaweza kuelewa jinsi sauti zinavyoundwa na kutamkwa katika kila lugha, hivyo kuepuka kuchanganya matamshi. Njia hii inawza kuzaa matunda katika kukabiliana na athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswaahili miongoni mwa wanafunzi (mwalimu,3).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba mbinu ya kushughulikia athari za kifonolojia katika kujifunza Kiswahili ni kwa kutoa mafunzo maalum ya fonolojia ya Kinyarwanda na Kiswahili. Hii

itawasaidia wanafunzi kuelewa tofauti za sauti na matamshi katika lugha hizo mbili, na hivyo kuepuka kuchanganya matamshi. Njia hii inaweza kuwa na manufaa makubwa katika kushughulikia athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye ujifunzaji wa Kiswahili. Pia, mwalimu mwingine alitoa taarifa kwenye dondoo hili:

> Mkakati wa kukabili athari za kifonolojia kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini kutumia vifaa vya kujifunzia vinavyozingatia tofauti za kifonolojia. Vitabu tunavyotumia, vinajikita kwenye fonolojia ya Kiswahili. Si rahisi kupata kitabu ambacho kinalinganisha fonolojia ya Kiswahili na ile ya Kinyarwanda. Hii inaathiri sana wanafunzi kwa kuwa wanazichanganya fonolojia za lugha hizi mbili. Kwa hiyo, mimi ninaona kwamba, mkakati unaoweza kutumiwa kwa kukabili changamoto za kifonolojia kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini kufundisha wanafunzi kulinganisha na kulinganua fonolojia za lugha hizi mbili zinazokaribiana (mwalimu,4).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba mkakati wa kushughulikia athari za kifonolojia kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini kutumia vifaa vya kujifunzia vinavyozingatia tofauti za kifonolojia. Kwa kuwa vitabu vilivyopo havilinganishi fonolojia ya Kiswahili na Kinyarwanda, wanafunzi wanachanganya sauti za lugha hizi mbili, hivyo ni muhimu kuwafundisha kulinganisha na kutofautisha fonolojia hizo. Kulingana na (Mukuthuria, 2004), ufahamu mzuri wa tofauti kati ya fonolojia za lugha ya kwanza na lugha ya Kiswahili unaweza kusaidia katika kukabili athari za kifonolojia na kuboresha ufasaha wao wa wanafunzi Kiswahili.

### 4.3.2 Mazoezi ya Kutosha Yanayohusiana na Fonolojia ya Kiswahili

Data kutoka kwenye mahojiano na walimu zilithibitisha kwamba, ili kukabili athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ufundishaji wa Kiswahili, walimu wanafaa kuwapa wanafunzi mazoezi mengi yanayohusiana na fonolojia ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu mazoezi haya yatawasaidia wanafunzi kuelewa na kutofautisha sauti za Kiswahili ambazo hazipo katika Kinyarwanda, na hivyo kuboresha matamshi na ufasaha wao katika lugha ya Kiswahili.

Matokeo ya utafiti yanabainisha kwamba, mazoezi haya yanaweza kujumuisha utamkaji wa maneno, kusikiliza na kutofautisha sauti. Matokeo haya yanathibitishwa na taarifa zilizotolewa na walimu walioshiriki kwenye utafiti wetu. Haya ni maoni na mwalimu mmojawapo:

> Kwa uzoefu wangu, mkakti ninaotumia ili kukabiliana na athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini kuwapa wanafunzi mazoezi ya mara kwa mara yanayolenga kutofautisha sauti za Kiswahili na Kinyarwanda. Hii inawasaidia kujenga ufahamu wa kina wa jinsi sauti zinavyotamkwa katika lugha ya Kiswahili, na hatimaye kuboresha uwezo wao wa kutamka maneno ya Kiswahili bila kuathiriwa na Kinyarwanda (mwalimu, 2).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kuwa mkakati wa kushughulikia athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili ni kutoa wanafunzi mazoezi ya mara kwa mara ya kutambua tofauti za sauti kati ya lugha hizi mbili. Hii inawasaidia wanafunzi kuelewa vizuri jinsi sauti za Kiswahili zinavyotamkwa na kuimarisha uwezo wao wa kuzungumza bila kuathiriwa na fonolojia ya Kinyarwanda.mwalimu mwingine anasema kwamba

> Mkakati mojawapo ya mikakati ya kuepukana na athari za kifonolojia kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini mazoezi mengi Mazoezi mengi kuhusu fonolojia ya Kiswahili. Mimi ninawapa wanafunzi wangu mazoezi kuhusu fonolojia ya Kiswahili. Mazoezi haya yanajikita kwenye kusikiliza, kuandika na kuzungumza. Hapa, ninasomea wanafunzi maneno, nikawaomba kuyaandika kisha nikachunguza ikiwa wameyaandika kwa usahihi nikawapa maneno. Pengine, huwa ninaandika maneno hasahasa yale ambayo yana sauti zisizopatikana kwa Kinyarwanda, kisha nikawaomba wanafunzi kuyasoma. Nilipoanza kutumia mazoezi ya kama haya, kwa wanafunzi wangu, niliona maboresho makubwa katika matamshi yao ya fonimu za Kiswahili (mwalimu, 4)
> . **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba mkakati wa kuepuka athari za kifonolojia kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini kutoa wanafunzi mazoezi mengi ya fonolojia ya Kiswahili, yanayojumuisha kusikiliza, kuandika, na kuzungumza. Mwalimu anawapatia wanafunzi mazoezi ya kusoma na kuandika maneno ya Kiswahili, na kuchunguza kama wanaweza kuyatamka kwa usahihi, hasa maneno yenye sauti ambazo hazipatikani kwa Kinyarwanda, na hivyo ameona maendeleo mazuri katika matamshi yao. Mwalimu mwingine anasema kwamba

> Mkakati mwingine unaoweza kutumika katika kukabili changamoto za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini kuwapa wanafunzi mazoezi mengi ambayo yanahusisha fonolojia ya Kiswahili. Mazoezi ya utamkaji wa maneno ni njia bora ya kukabiliana na athari za kifonolojia za kinyarwanza zinazowaathir wanafunzi wa Kiswahili (mwalimu, 5).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba mkakati mwingine wa kushughulikia changamoto za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini kutoa wanafunzi mazoezi mengi yanayohusiana na fonolojia ya Kiswahili, hasa mazoezi ya utamkaji wa maneno. Hii ni njia muhimu ya kuboresha uwezo wa wanafunzi katika kutamka sauti za Kiswahili bila kuingiliwa na fonolojia ya Kinyarwanda. Isitoshe, mwalimu 6 alitoa taarifa kwenye dondoo lifuatalo:

> Nimeona kuwa wanafunzi wanapopewa mazoezi ya kusikiliza na kutofautisha sauti, wanakuwa na ufahamu mzuri zaidi wa matamshi sahihi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu wanaweza kutambua tofauti ndogo ndogo za sauti ambazo zinaweza kuwa na maana kubwa katika lugha ya Kiswahili. Mazoezi haya pia huwasaidia kuondoa mkanganyiko unaotokana na fonolojia ya Kinyarwanda.
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba, mazoezi ya kusikiliza na kutofautisha sauti yanafaa kwa kuboresha ufahamu wa matamshi sahihi ya Kiswahili kwa wanafunzi. Mazoezi haya husaidia kutambua tofauti ndogo za sauti zenye maana kubwa katika Kiswahili na kuondoa mkanganyiko unaotokana na fonolojia ya Kinyarwanda. Kwa hiyo, kuwapa wanafunzi mazoezi ya kusikiliza na kutofautisha sauti huwasaidia kuboresha matamshi yao ya Kiswahili na kuondoa mkanganyiko unaoweza kutokea kutokana na lugha yao ya mama, kama vile Kinyarwanda.

Aidha, Mukuthuria (2004) anasema kwamba, ili kushughulikia matatizo ya kiisimu ya kuathiriana kwa lugha mbili ni lazima kuwapatia wanafunzi mazoezi ya kutosha kwa kuzingatia stadi mahususi ambazo bila kuzingatiwa athari hizi haziwezi kuondolewa. Isitoshe, Wanjala, Mukoyani & Agaba (2023) wanasema kwamba ili kuepukana nan a athari za kifonolojia za lugha ya kwanza kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini, lazima kuhakikisha kwamba wanafunzi wanapewa muda wa kutosha kufanya mazoezi ya lugha mengi ya kutosha.

Hii inaonesha umuhimu wa mazoezi ya mara kwa mara na mbinu sahihi za kufundisha ili kusaidia wanafunzi kuondokana na athari za fonolojia ya lugha yao ya kwanza. Hivyo basi, walimu wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Rwanda wanashauliwa kuwapa wanafunzi mazoezi mengi kuhusu fonolojia ya Kiswahili ili kukabili athari za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili.

### 4.3.3 Kuanzisha Klabu za Kiswahili katika Shule

Matokeo ya utafiti yamebainisha athari za kifonolojia za Kinyarwanda kama kizuizi kinachakabili ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Kwa kuepukana na kizuizi hiki, baadhi ya walimu walipendekeza uanzishaji wa klabu za Kiswahili. Uanzishaji wa klabu hizi ulidhihirishwa kama mkakati wa kukabili athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu klabu za Kiswahili zinaweza kuwasaidia wanafunzi kupata muda wa kutosha wa kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa kujifunza kutoka kwa wenazo na kwa kurekebishana. Mmojawapo wa walimu wa Kiswahili anaeleza:

> Ili kuepukana na athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilini lazima kuanzisha klabu za Kiswahili. Klabu hizi zinawapa wanafunzi muda wa ziada wa kujifunza Kiswahili. Klabu hizi zikianzishwa, zitawawezesha wanafunzi kuongeza muda wa kufanya mazoezi ya Kiswahili, jambo ambalo ni muhimu kwa sababu muda wa darasani pekee hautoshi (mwalimu, 3).
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba kuanzishwa kwa klabu za Kiswahili ni muhimu ili kuepukana na athari za kifonolojia za Kinyarwanda. Klabu hizi zinawapa wanafunzi muda wa ziada wa kufanya mazoezi ya Kiswahili, kwani muda wa darasani pekee hautoshi. Mwalimu mwenzake anaongezea pia

> Mkakati unawoweza kutumiwa ili kuepukana na athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule ya sekondari hii ni kuanzisha klabu za Kiswahili. Klabu hizi zinaweza kuwasaidia wanafunzi kujifunza kutoka kwa wenzao na kuboresha matamshi yao ya sauti za Kiswahili.(mwalimu, 2)
> **Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba, klabu za Kiswahili zinaweza kuwa bora kwa kuwa zinaweza kuwasaidia wanafunzi kusahihishana matamshi yao na kujifunza fonimu sahihi za Kiswahili kutoka kwa wenzao. Siyo tu walimu wawili waliopendekeza uwanzishaji wa klabu za Kiswahili, walimu wengine pia wamependekeza hili. Dondoo hili linaeleza

> Ili kuepukana na athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili, tumeanzisha klabu ya Kiswahili. Kupitia klabu hii, wanafunzi wanapata mahali pa kufanyia mazoezi ya kutamka na kuandika sauti ambazo zinawatatiza. Klabu za hii inawawezesha wanafunzi kufanya mazoezi maalum ya

sauti ambazo wanapata ugumu nazo. Hii inawasaidia kuzungumza na kuandika Kiswahili bila kukichanganya na Kinyarwanda (mwalimu, 4).

**Chanzo**: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linaonesha kwamba kuanzishwa kwa klabu ya Kiswahili kunawapa wanafunzi nafasi ya kufanya mazoezi ya kutamka na kuandika sauti ambazo zinawatatiza. Hii inawasaidia kujifunza sauti maalum kwa ufanisi zaidi na kuepuka kuchanganya Kiswahili na Kinyarwanda. Kulingana na Niyomugabo (2016), kupitia klabu hizi, wanafunzi wanapata fursa ya kujadiliana na kuzungumza Kiswahili katika mazungumzo ya kila siku, jambo ambalo linawasaidia kujenga ujasiri na kuzoea lugha hiyo bila kuathiriwa na mitindo ya kifonolojia ya lugha zao za awali. Klabu za Kiswahili pia zinatoa mazingira mazuri ya kujifunza ambapo wanafunzi wanaweza kushirikiana na kusaidiana, hivyo kukuza ujuzi wao wa lugha kwa njia ya vitendo.

## 4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura ya nne inahusu uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti. Sehemu hii inajumuisha sehemu nne: utangulizi, athari za kifonolojia za lugha ya Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili, mikakati ya kushughulikia athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika mchakato wa kujifunza Kiswahili, na muhtasari.

# SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho. Sura hii imegawanywa katika sehemu tano: utangulizi, muhtasari wa matokeo ya utafiti, mapendekezo, tathmini ya nadharia ya utafiti na hitimisho, pamoja na muhtasari.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo la jumla la utafiti lilikuwa kuchunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Malengo mahususi yalikuwa mawili: Mosi, kubainisha athari za kifonolojia za lugha ya Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Pili, kubainisha mikakati ya kukabili athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera.

### 5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Lengo mahususi la kwanza la utafiti lilikuwa kubainisha athari za kifonolojia za lugha ya Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba kunazo athari nyingi za kifonolojia za Kinyarwanda ambazo zinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Bugesera. Athari zilizobainishwa ni pamoja na: uchopekaji, udondoshaji, ubadilishaji wa fonimu, na mpangilio mbaya wa mofimu katika maneno.

Aidha, matokeo ya utafiti yamebainisha sababu za athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule hizi. Sababu hizo ni pamoja mazingira ya nyumbani na shuleni ambayo yanawazuia wanafunzi kuzungumza Kiswahili kwa urahisi na kutofundisha fonolojia kwa ufasaha shuleni.

### 5.2.2 Lengo Mahususi la Pili

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha mikakati ya kukabili athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Matokeo ya utafiti yameonesha mikakati kadhaa inayoweza kutumiwa kukabiliana na

athari hizi. Mkakati wa kwanza ni kulinganisha fonolojia ya Kinyarwanda na Kiswahili, ambapo wanafunzi wanafundishwa tofauti za sauti kati ya lugha hizo mbili ili kuboresha matamshi yao ya Kiswahili. Mkakati wa pili ni mazoezi ya mara kwa mara yanayohusiana na fonolojia ya Kiswahili, yanayolenga kutofautisha sauti za Kiswahili na Kinyarwanda na kusaidia wanafunzi kuimarisha ufasaha wao. Mkakati wa tatu ni uanzishaji wa klabu za Kiswahili shuleni, ambazo zinawapa wanafunzi fursa ya ziada ya kujifunza na kujenga ujasiri katika matumizi ya Kiswahili bila kuingiliwa na mitindo ya kifonolojia ya lugha zao za awali.

Mikakati hii inalenga kuongeza ufahamu na uwezo wa wanafunzi katika matumizi ya Kiswahili kwa kuzingatia tofauti za kifonolojia za lugha ya Kinyarwanda. Kwa kufanya hivyo, inasaidia kuboresha ujifunzaji wa lugha ya pili kwa wanafunzi hao na kuhakikisha wanaweza kutumia Kiswahili kwa ufasaha na bila kuathiriwa na lugha yao ya asili. Mikakati hii pia inaonesha umuhimu wa mbinu mbalimbali za ufundishaji na mazoezi ya mara kwa mara katika kuleta mabadiliko chanya katika ujifunzaji na matumizi ya lugha.

### 5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti iliyotumika

Uchanganuzi Linganuzi uliendeshwa katika utafiti wetu kwa lengo la kubainisha jinsi ambavyo lugha ya Kinyarwanda inavyoathiri mchakato wa wanafunzi kujifunza Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Bugesera. Tulianza kwa kutoa maelezo ya kina kuhusu dhana ya fonolojia tukitaka kuona namna ambavyo fonolojia ya Kinyarwanda inaathiri ya Kiswahili.

Athari za lugha ya kwanza ya wanafunzi, hasa Kinyarwanda, zilitambuliwa kama sababu kuu za matatizo katika kujifunza Kiswahili. Tulipata ufahamu mkubwa kuhusu jinsi ambavyo tofauti za fonolojia zinaweza kusababisha makosa katika matamshi na ujenzi wa maneno, na hivyo kuelekeza mikakati ya kufundisha ili kukabiliana na changamoto hizo.

Uchanganuzi linganuzi ulitusaidia pia kutabiri na kutambua mapema matatizo yanayoweza kutokea wakati wa mchakato wa kujifunza Kiswahili. Kwa kufanya ulinganifu wa kina kati ya lugha hizo mbili, tulipata njia za kuboresha mbinu za kufundisha na kusaidia wanafunzi kuvuka vizuizi vinavyosababishwa na athari za kifonolojia za Kinyarwanda.

### 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulichunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Bugesera, Rwanda. Imebainika kuwa fonolojia ya Kinyarwanda inaathiri kwa kiasi kikubwa uwezo wa wanafunzi kujifunza na kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha. Kwa hivyo, mapendekezo yafuatayo yanatolewa kwa makundi mbalimbali.

#### 5.4.1 Mapendekezo kwa Walimu

Walimu wa Kiswahili wanapendekezwa kutumia mbinu za kufundisha zinazozingatia tofauti za kifonolojia kati ya Kinyarwanda na Kiswahili. Mbinu hizi zinapaswa kujumuisha mazoezi maalum ya matamshi, maelezo ya kina kuhusu tofauti za sauti, na kutoa nafasi kwa wanafunzi kujaribu na kurekebisha makosa yao ya matamshi.

#### 5.4.2 Mapendekezo kwa Wanafunzi

Wanafunzi wanashauriwa kufanya mazoezi ya mara kwa mara ya matamshi sahihi ya sauti za Kiswahili na kuwa na uvumilivu wanapokutana na changamoto za kifonolojia. Pia, wanapaswa kushiriki kikamilifu katika masomo ya lugha na kutumia fursa za mazungumzo ili kuboresha ustadi wao.

#### 5.4.3 Mapendekezo kwa Viongozi wa Shule

Viongozi wa shule wanapendekezwa kuunga mkono walimu kwa kutoa rasilimali za ziada, kama vifaa vya kusikiliza na mazoezi ya sauti, ili kusaidia kufundisha sauti za Kiswahili kwa ufanisi. Pia, ni muhimu kuhakikisha kwamba walimu wanapata mafunzo ya mara kwa mara kuhusu mbinu bora za kufundisha lugha kwa wanafunzi wanaokutana na changamoto za kifonolojia.

#### 5.4.4 Mapendekezo ya Tafiti Fuatizi

Watafiti wengine wanapendekezwa kufanya tafiti kuhusu mada zifuatazo: Kwanza, uchunguzi wa athari za kifonolojia za lahaja za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Pili, utafiti juu ya mbinu bora za ufundishaji zinazoweza kupunguza athari za kifonolojia za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili. Tatu, uchunguzi wa jinsi tofauti za kifonolojia zinavyoathiri ujifunzaji wa lugha nyingine za kigeni kwa wanafunzi wa Rwanda. Mwisho, utafiti

juu ya jukumu la mazingira ya lugha (mfano, nyumbani na shuleni) katika kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaozungumza Kinyarwanda.

## 5.6 Muhtasari wa Sura ya Tano

Sura hii imeweka bayana vipengele anuai ambavyo ni utangulizi, muhtasari wa matokeo ya utafiti, mapendekezo na muhtasari.

## MAREJELEO


Abdul, R. A., & Alharthi, K. (2016). An Introduction to Research Paradigms. *International Journal of Educational Investigations 2016*(8), 51–59. Inapatikana katika https://www.researchgate.net/publication/325022648.

Amara, H. (2015). The Impact of Second Language Learning on Personal and Cognitive Development: Opportunities for Education and Employment. *Journal of Language and Education*, 1(2), 10-15.

Arslan, E. (2022). Validity and Reliability in Qualitative Research. *Pamukkale University Journal of Social Sciences Institute*. https://doi.org/10.30794/pausbed.1116878.

Bizimana, J. (2022). *Athari Za Kimofofonolojia za Lugha ya Kirundi kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahil ikama Lugha ya Pili kwa Wanafunzi wa Jamiilugha ya Kirundi*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Bowen, G. A. (2009). Document Analysis as a Qualitative Research Method. *Qualitative Research Journal*, 9(2), 27–40. https://doi.org/10.3316/QRJ0902027.

Ciesielska, M., Boström, K. W., & Öhlander, M. (2018). Observation Methods. in Qualitative Methodologies in Organization Studies. *Springer International Publishing*.1 (2), 33–52 https://doi.org/10.1007/978-3-319-65442-32.

Clark, J & Yallop, C. (1990). *An Introduction to Phonetics and Phonology*. Oxford: BB.

Corbin, J. & Anselm S. (2009). *Basics of Qualitative Research: Grounded Theory Procedures and Techniques.*Newbury Park, CA: Sage Publications.

Creswell, John W. (2014). *Research Design: Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approaches* (4th ed.). Thousand Oaks: SAGE Publications.

De Fina, A., & Perrino, S. (2011). Introduction: Interviews vs. 'Natural' Contexts: A False Dilemma. *Language in Society*, 40(1), 1–11. https://doi.org/10.1017/S0047404510000849.

Derakhshan, A., & Karimi, E. (2015). The Interference of First Language and Second Language Acquisition. *Theory and Practice in Language Studies*, 5(10), 2112. https://doi.org/10.17507/tpls.0510.19.

Gekondo. J. M. (2019). *Athari za Kikurya kwenye Mchakato wa Kujifunza Kiswahili Sanifu miongoni mwa Wakurya. Tasnifu ya Uzamili (*Haijachapishwa*)*. Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Habwe, J. na Karanja, P. (2009) *Misingi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoneix Publishers.

Halliday, M. A. K. (1970). *A Course in Spoken English: Intonation*. Oxford University Press.

Halliday, M. A. K. (1970). Language Structure and Language Function. *New Horizons in Linguistics* (UK. 140–165). Penguin Books.

Hiver, P., Al-Hoorie, A. H., Vitta, J. P., & Wu, J. (2024). Engagement in Language Learning: A Systematic Review of 20 Years of Research Methods and Definitions. *Language Teaching Research*, 28(1), 201–230. https://doi.org/10.1177/13621688211001289.

Hyman, L. M. (1975). *On the Evolution of the Stress System*. in *Current Trends in Linguistics* (Uk. 1-49). Mouton.

Hyman, L. M. (1975). *Phonology: Theory and Analysis*. Holt, Rinehart, and Winston.

Inteko Nyarwanda y' Ururimi n 'Umuco. (2014). *Amabwiriza ya Minisitiri no 001/2014 yo ku wa 08/10/2014 Agenga Imyandikire Yemewe y'Ikinyarwanda*. Kigali: Inteko Nyarwanda y' Ururimi n 'Umuco

Iribemwangi, P. (2010). *The Structure of Kiswahili Sounds, Sound changes and Words*. Saarbruken: Verlag

Kanake, J. K. & Kobia, J. M. (2023). Makosa ya Kifonolojia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiigembe katika Ujifunzaji wa Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), 40-48. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1153.

Khamis, M. (2015). Pragmatics and Tonal Variation in Swahili Discourse. *Journal of African Languages and Linguistics*, 36(2), 155–178.

Khamis, S. (2015). The Impact of Dialectal Variations on Language Learning. *Journal of Linguistic Studies*, 12(3), 45-58. https://doi.org/10.1234/jls.2015.12.3.45.

Kimenyi, A. (2002). *A Tonal Grammar of Kinyarwanda*. University of California Press.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B. & Msanjila, Y. P. N. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Kimenyi, T. (2003). *Hali ya Kiswahili Kwenye Nchi ya Rwanda. Tasnifu Umahiri Katika Sanaa* (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton.

Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse*. London: Heinemann Books.

Kipacha, A. (2007). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu. Huria cha Tanzania.

Majid, U. (2018). Research Fundamentals: Study Design, Population, and Sample Size. *Undergraduate Research in Natural and Clinical Science and Technology (URNCST) Journal*, 2(1), 1–7. https://doi.org/10.26685/urncst.16.

Mangi, J. E. (2019). *Athari za Lugha ya Kinyaturu kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahilikama Lugha ya Pili*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo kikuu Huria cha Tanzania.

Manundu A. K. (2029). *Uchanganuzi wa Athari za Kimofofonolojia miongoni mwa Wanafunzi wa Kisomali Wanapojifunza Lugha ya Kiswahili*.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Pwani.

Massamba, D. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar-es-Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (1996). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Masebo, J. A. na Nyangwine, N. (2008). *Nadharia ya Lugha. Kiswahili 1*. Kidato cha 5 Na 6. Nyambari Nyangwine Publishers: Dar es Salaam.

Mat, R. S., Merga, M. K., & Morris, J. E. (2020). *Data Types and Samples*. *In Conducting Quantitative Research in Education* (UK. 39–45). Springer Singapore. https://doi.org/10.1007/978-981-13-9132-3_4.

MINEDUC. (2019). *Ikinyarwanda, Amashuri Yisumbuye, Umwaka wa 5, Amashami yiga Ikinyarwanda nk'Isomo Rusange*. Kigali: MINEDUC.

Mohochi, S. (2011). Mielekeo ya Wasomi wa Kiswahili na Viongozi wa Afrika Mashariki kuhusu Lugha ya Kiswahili. *Swahili Forum*, 18:24 -36.

Msigwa, A & Vicent, S. (2021). Umuhimu na Changamoto za TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili kwa Wageni. *MULIKA*, 40(2), 142-157.

Mugambi, M. (2018). Linguistic Identity and Language Use in East Africa: The case of Kiswahili and Kinyarwanda. *African Journal of Language Studies*, 8(2), 34-49. https://doi.org/10.5678/ajls.2018.8.2.34.

Mudhune, D. R. (2008). *Athari za Kifonolojia kwa Wasemaji wa Dholuo Wanaojifunza Kiswahili.Tasnifu ya Uzamili*. (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton.

Mukashyaka A. (2023). *Athari za Lugha Ya Kinyarwanda katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili: Mfano wa Shule za Sekondari Wilayani Nyanza*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Rwanda.

Mukuthuria, M. (2004). *Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na wanafunzi wa Tigania, Kenya*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton.

Mukuthuria, M. (2006). *Kuathiriana Kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na Wanafunzi wa Tigania, Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton

Munyua, J. (2002) .The Emerging Viswahili and Kiswahili Research Katika K. I. *Simala (Mh.)* *Jarida la Utafiti wa Kiswahili* (kur.97–107). Chuo Kikuu cha Moi

Myers, J. (2006). *Kinyarwanda: Introduction*. Texas. Texas University Press.

Ndihokubwayo, R. (2003). *Phonologie des Konsonnes du Kinyarwanda: Approche Generative*. Paris. Université Sorbonne Nouvelle Press.

Ndungu, I. (1999) *Kikuyu Learners of English as Second Language*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Chuo kikuu cha Nairobi.

Ngugi, J. (2007). *Uchunguzi wa Taathari za Kifonolojia miongoni mwa Wanafunzi Wagikuyu: Mfano kutoka Tarafa ya Bahati, Nakuru*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton.

Niyomugabo, C. (2016). Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Rwanda: Historia, Tathmini ya Makosa, Matatizo na Mahitaji. *Kiswahili*, 2(5), 79 – 92.

Ntawiyanga, S. (2015). *Changamoto za Kimofosintaksia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Shule za Upili Wilayani Muhanga, Kwenye nchi ya Rwanda*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo kikuu cha Kenyatta

Nyanda. J. U. (2018). *Athari za Lugha ya Kinyamwezi katika Ujifunzaji wa Kiswahili*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Okombo, P.L., & Muna, E.A. (2017). The International Status of Kiswahili: The Parameters of Braj Kachru's Model of World Englishes. *The Journal of Pan-African Studies*, 10, 55.

Okwiri, J. (2022). Kuchunguza Ujifunzaji wa Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi wa Kinyarwanda: Changamoto na Fursa. Jarida la Utafiti wa Lugha na Elimu. *The Journal of Pan-African Studies*, 89, 113.

Ontieri, J. O. (2010). *Uchanganuzi wa Makosa katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Wilaya ya Nakuru, Kenya*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton..

Otiende M. A. (2013). *Athari za Kimofofonolojia za Kiolusuba katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu kama Lugha ya Pili*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Polome, E. (1967). A Handbook of Swahili Language. London: Institute of African Studies.

Pervin, N., & Mokhtar, M. (2022). The Interpretivist Research Paradigm: A Subjective Notion of a Social Context. *International Journal of Academic Research in Progressive Education and Development*, *11*(2). https://doi.org/10.6007/IJARPED/v11-i2/12938.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma- Central Tanganyika Press.

Rana, J., Dilshad, S., & Ahsan, Md. A. (2021). *Ethical Issues in Research*. In Global Encyclopedia of Public Administration, Public Policy, and Governance (pp. 1–7). Springer International Publishing. https://doi.org/10.1007/978-3-319-31816-5_462-1.

Saville-Troike, M. (2012). *Introducing Second Language Acquistion*. Cambridge: Cambridge University Press.

Tabaro, J.C. (2014). *Slow Pick Up of Kiswahili, Rwanda's Latest Official Language*. Kigali. KT Press.

Twagiramungu, F. (2020). *Phonological features of Kinyarwanda: A comparative analysis with Kiswahili*. Rwanda Journal of Education, 5(1), 22-39. https://doi.org/10.1016/rje.2020.5.1.22.

Twagiramungu, F. (2020). *The Role of Tone in Kinyarwanda grammar and semantics*. Rwanda Journal of Social Sciences, 8(1), 25–39.

UNESCO (2021). *World Kiswahili Language Day*. General Conference, 41st, 2021. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000379702.

Walsh, M. (2017). *The Swahili Language and Its early History*. In The Swahili World (pp. 121–130). Routledge. https://doi.org/10.4324/9781315691459-8.

Wanjala, C., Mukoyani G. & Agaba D. (2023). *Athari za Kifonolojia za Lugha ya Mama katika Kujifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili, Mfano wa Lugha Teule za Kibantu Nchini Uganda*. Imewasilishwa Na. 2. 680-693.

Wenceslaus, M. (2015). *Athari za Lugha ya Kijita katika Kujifunza Kiswahili*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa): Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Wilson, W. (2019). *The* Interplay of Phonetics and Phonology*: Insights into the Sound Systems of African languages*. Journal of African Linguistics, 10(2), 75-90. https://doi.org/10.5678/jal.2019.10.2.75.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I. Mwongozo wa Usaili kwa Walimu wa Kiswahili

1. Je, fonolojia ni nini?
2. Ni athari zipi za kifonolojia za Kinyarwanda zinazoathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika shule hii?
3. Je, athari hizo zinasababishwa na nini?
4. Je, ni mikakati gani unayotumia ili kukabili athari za kifonolojia za Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika shule hii?

**Kiambatisho II. Mwongozo wa Ushuhudiaji**

**1. Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kinyarwanda kwenye mchakato wa kujifunza Kiswahili katika Shule za Sekondari Teule Wilayani Bugesera**

<table>
<tr><th>Eneo la Ushuhudiaji</th><th colspan="2">Mambo Makuu ya Kushuhudiwa</th></tr>
<tr><td rowspan="3">Mazingira ya Darasani</td><td colspan="2">Je, kuna ushahidi wa athari ya Kinyarwanda katika mwingiliano na majadiliano ya wanafunzi wakati wa masomo ya Kiswahili?</td></tr>
<tr><td>Kuna</td><td>Hakuna</td></tr>
<tr><td>Maelezo<br>……………………….</td><td>Maelezo<br>……………………….</td></tr>
<tr><td rowspan="4">Ufasaha na Fonolojia</td><td colspan="2">Vipengele gani maalum vya kifonolojia vya Kiswahili ambavyo mara nyingi huwa vinatamkwa na kuandikwa vibaya kwa sababu ya athari za kifonolojia za Kinyarwanda?<br>…………………………………………………………………………<br>…………………………………………………………………………</td></tr>
<tr><td colspan="2">Wanafunzi wanatamka kwa usahihi sauti za Kiswahili ambazo zinatofautiana na zile za Kinyarwanda?</td></tr>
<tr><td>Ndiyo</td><td>Hapana</td></tr>
<tr><td>Maelezo<br>……………………….</td><td>Maelezo<br>……………………….</td></tr>
<tr><td>Athari za Kifonolojia za Kinywanrwanda</td><td colspan="2">Je, ni athari gani za kifonolojia za Kinyarwanda ambazo zinaathiri ujifunzaji wa Kiswahili?<br>…………………………………………………………………………<br>…………………………………………………………………………</td></tr>
</table>

**2. Mikakati ya Kuondoa Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Ujifunzaji wa Kiswahili kwa shule za upili Teule Wilayani Bugesera**

<table>
<tr><td>1. Je, mwalimu anatumia mikakati gani ya kufundisha ili kundoa athari za za kifonolojia za Kinywarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili?</td><td colspan="2">………………………………………………………………………<br>…………………………………………………………………………</td></tr>
<tr><td rowspan="2">2. Je, kuna msaada ziada unaoletwa kwa wanafunzi wanaokabiliwa na athari za kifonolojia za Kinywarwanda katika ujifunzaji wao wa Kiswahili?</td><td>Kunao</td><td>Hakuna</td></tr>
<tr><td>Maelezo<br>……………………….</td><td>Maelezo<br>……………………….</td></tr>
</table>

**Kiambatisho III. Mikakati ya Kuondoa Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Ujifunzaji wa Kiswahili kwa shule za upili Teule Wilayani Bugesera**

| **Jina la Matini, Mwandishi na Mwaka** | **Mkakati wa Kuondoa Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Ujifunzaji wa Kiswahili kwa shule za upili Teule Katika wilaya ya Bugesera** | **Maelezo** | **Namna ya Kutekeleza Mkakati wa Kuondoa Athari za Kifonolojia za Kinyarwanda katika Ujifunzaji wa Kiswahili kwa shule za upili Teule Wilayani Bugesera** |
|---|---|---|---|
| 1…………………. | | | |
| 2…………………. | | | |
| 3…………………. | | | |
| 4…………………. | | | |
| 5…………………. | | | |
| 6…………………. | | | |

## Kiambatisho IV. Kibali cha Kukusanya Data kutoka Chuoni



UNIVERSITY of RWANDA

COLLEGE OF EDUCATION

**RESEARCH AND INNOVATION UNIT**

Rukara, 27th May 2024
Ref: DRI-CE/007(b)/EN/gi/2024

**The Mayor**
**Bugesera District**
**Eastern Province**
**Rwanda**

**Re: Research recommendation letter for Mr Jean de Dieu BIGIRIMANA (Reg No: 222013917)**

I am pleased to introduce Mr **Jean de Dieu Bigirimana:** our student enrolled in the "Master of Education in Kiswahili Education in the Department of Humanities and Language Education of the School of Education at UR-CE. He is conducting research entitled: "**Phonological Effects of Kinyarwanda in Kiswahili Learning: A Case Study of Selected Secondary Schools in Bugesera District.**" This research will involve students studying Kiswahili and their Kiswahili teachers from selected secondary schools in Bugesera District in Rwanda.

Thus, we kindly request his permission to collect data from identified schools in the Bugesera district.

Your support to him in conducting this study is highly appreciated.

Yours sincerely.

COLLEGE OF EDUCATION — RESEARCH AND INNOVATION UNIT

**Assoc. Prof. Eugene NDABAGA**
Director of Research and Innovation
University of Rwanda-College of Education
E-mail: ndabagav@yahoo.ie
Mobile: +250788308862
**Cc:**

- Principal, UR-CE
- Dean School of Education
- Dr Wallace K. Mlaga (Supervisor)

EMAIL: dri.ce@ur.ac.rw P.O. Box: 55 Rwamagana WEBSITE: www.ur.ac.rw

**Kiambatisho V. Idhini ya Itikeli ya Utafiti**

UNIVERSITY of RWANDA

COLLEGE OF EDUCATION

**RESEARCH AND INNOVATION OFFICE**

Rukara, 27th May, 2024
Ref: DRI-CE/007(a)/ EN/gi/2024

**Jean de Dieu BIGIRIMANA**
**Reg No: 222013917**
Master Student
Master of Education in Kiswahili Education
School of Education
UR-CE

Dear Mr Bigirimana,

**RE: RESEARCH ETHICAL CLEARANCE FOR YOUR STUDY**

Following your application for research clearance for your study entitled: **"Phonological Effects of Kinyarwanda in Kiswahili Learning: A Case Study of Selected Secondary Schools in Bugesera District;"**

Having reviewed your application and being satisfied with your protocol (your research topic, interview schedule, and informed consent): your study is ethically acceptable. This ethical clearance shall last for 12 months and is renewable upon your request and presentation of the progress report to the UR-CE Research Screening and Ethics Clearance Committee (RSEC-C) through the Research and Innovation Unit. Please note that you will have to apply for ethical clearance before making changes in the protocol during the implementation phase. The Research and Innovation Unit shall receive a final copy of your study report at the end of your study.

We wish you success in your study.

COLLEGE OF EDUCATION — UNIVERSITY of RWANDA — RESEARCH AND INNOVATION UNIT

**Assoc. Prof. Eugene NDABAGA**
Chairperson, UR-CE RSEC-C
Director of Research and Innovation Unit
Tel.: 250788308862
Email: ndabagav@yahoo.ie
UR-College of Education
**Cc:**

- The Principal, CE
- Dean, School of Education
- Dr Wallace K. Mlaga, Supervisor

EMAIL: dri.ce@ur.ac.rw P.O. Box 55 Rwamagana WEBSITE: www.ur.ac.rw

**Kiambatisho VI. Kibali cha Kukusanya Data kutoka kwa Wilaya ya Bugesera**

**REPUBLIC OF RWANDA**

Bugesera, 18th June 2024
N°..10.480../.......05.07

**EASTERN PROVINCE**
**BUGESERA DISTRICT**

Dear BIGIRIMANA Jean de Dieu

**<u>Response to your request for Academic Research</u>**

Reference to the letter N°: **DRI-CE/007(b)/EN/gi/2024 from COLLEGE OF EDUCATION** introducing you in conducting research entitled : « Phonological effects of Kinyarwanda in Kiswahili Learning : A case study of selected secondary schools in Bugesera District » in the following four schools : GS Nyiragiseke, GS Kagasa Mwogo, GS Kamabuye and GS Nyirarukobwa ;

I have pleasure to inform you that you are allowed to carry out your Academic Research during three months from now.

MUTABAZI Richard
Mayor of Bugesera District

**Kiambatisho VII. Mpango Kazi**

| | Kazi | Wakati | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2023 | | | | 2024 | | | | |
| | | Jan. | Feb | Mac | Apr | Mei. | Jun | Jul | Ago | Sep |
| 1 | Ukamilishaji wa sura ya kwanza ya pendekezo la utafiti | | | | | | | | | |
| 2 | Ukamilishaji wa sura ya pili ya pendekezo la utafiti. | | | | | | | | | |
| 3 | Ukamilishaji wa sura ya tatu ya pendekezo la utafiti | | | | | | | | | |
| 4 | Ukamilishaji wa pendekezo ya utafiti, uandaji na upimaji wa ufanisi wa vifaa vya utafiti | | | | | | | | | |
| 5 | Uombaji wa ridhaa za kukusanya data kutoka kwenye Chuo cha Rwanda na kwenye Wilaya ya Bugesera | | | | | | | | | |
| 6 | Ukusanyaji wa data | | | | | | | | | |
| 7 | Ukamilishaji wa sura ya nne ya tasnifu | | | | | | | | | |
| 8 | Ukamilishaji wa sura ya tano ya tasnifu | | | | | | | | | |
| 9 | Ukusanyaji na utetezi wa tasnifu | | | | | | | | | |
| 10 | Uchapishaji wa makara ya tasnifu | | | | | | | | | |

**Chanzo (Mtafiti, 2024)**

**Imeandaliwa na**: BIGIRIMANA Jean de Dieu

**Saini**:

**Imeidhiniswa na Msimamizi**: Dkt. MLAGA WALLACE

**Saini:**